RASIMU YA 2

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

# SERA YA ELIMU NA MAFUNZO 2010

(Toleo Jipya) MACHI, 2011

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ADEM | Agency for Development of Education Management |
| AZAKI | Asasi za Kiraia |
| DED | District Executive Director |
| DEO | District Eduction Officer |
| EAC | East African Community |
| EFA | Education For All |
| EMAC | Educational Materials Approval Committee |
| ESDP | Education Sector Development Programme |
| EWW | Elimu ya Watu Wazima |
| ENMRA | Elimu Nje ya Mfumo Rasmi |
| HESLB | Higher Education Students' Loans Board |
| KCM | Kisomo Chenye Manufaa |
| KCK | Kisomo Cha Kujiendeleza |
| KKK | Kusoma, Kuandika na Kuhesabu |
| MDGs | Millenium Development Goals |
| MEMKWA | Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa |
| MKUKUTA | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania |
| MMEJU | Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu |
| MMEM | Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi |
| MMES | Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari |
| MMEU | Mpango wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi |
| MUKEJA | Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya watu wazima na Jamii |
| NACTE | National Council for Technical Education |
| NECTA | National Examinations Council of Tanzania |

| | |
|---|---|
| NER | Net Enrolment Ratio |
| NEQA | National Education Qualifications Authority |
| NEQF | National Education Qualifications Framework |
| OWM-TAMISEMI | Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| RAS | Regional Administrative Secretary |
| REO | Regional Education Officer |
| SADC | Southern Africa Development Community |
| SDL | Skills Development Levy |
| TEA | Tanzania Education Authority |
| TCU | Tanzania Commission for Universities |
| TDMS | Teachers Development and Management Strategy |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TEWW | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| TIE | Tanzania Institute of Education |
| TLSB | Tanzania Library Services Board |
| TSD | Teachers Service Department |
| TVET | Technical and Vocational Education and Training |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| UN | United Nations |
| UNDP | United Nations Development Programme |
| UNESCO | United Nations Educational Scientific and Cultural Organisation |
| UPE | Universal Primary Education |
| VET | Vocational Education and Training |
| VETA | Vocational Education and Training Authority |
| VVU | Virusi vya Ukimwi |

YALIYOMO

VIFUPISHO ........................................................................................ i
YALIYOMO ........................................................................................ iii
DIBAJI ........................................................................................ v

SURA 1 ........................................................................................ 1
1.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 1

SURA YA 2 ........................................................................................ 3
2.0 HALI YA UTOAJI WA ELIMU NA ELIMU NA MAFUNZO NCHINI .. 3
2.1 Utoaji wa Elimu na Mafunzo Tangu Uhuru ........................................ 3
2.2 Mfumo na Muundo wa Elimu na Mafunzo ........................................ 5
2.3 Mafanikio ........................................................................................ 8
2.4 Changamoto ........................................................................................ 9

SURA 3 ........................................................................................ 10
3.0 UMUHIMU WA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO ............................ 10
3.1 Usuli ........................................................................................ 10
3.2 Mabadiliko yaliyojitokeza katika utekelezaji wa Sera za Elimu na Mafunzo ............ 10

SURA 4 ........................................................................................ 12
4.0 FALSAFA, DIRA, DHIMA NA MADHUMUNI YA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO .......... 12
4.1 Falsafa ya Elimu na Mafunzo ........................................ 12
4.2 Dira ........................................................................................ 12
4.3 Dhima ........................................................................................ 12
4.4 Madhumuni ya Sera ya Elimu na Mafunzo ........................................ 13
4.4.1 Madhumuni ya Jumla ........................................................................ 13
4.4.2 Madhumuni Mahsusi 14
SURA YA 5 ........................................................................................ 15
5.0 HOJA ZA SERA NA MATAMKO ........................................ 15
5.1 Mfumo wa Elimu na Mafunzo 16
5.2 Muundo wa Elimu na Mafunzo ........................................ 16
5.3 Fursa na Usawa katika Utoaji wa Elimu na Mafunzo .......................... 27
5.4 Mitaala ya Elimu na Mafunzo ........................................ 33
5.5 Lugha katika Elimu na Mafunzo. ........................................ 37

5.6 Upimaji, Tathmini na Utoaji Vyeti....................................................42
5.7 Uongozi na Utawala wa Elimu na Mafunzo........................................44
5.8 Uwezo katika Utoaji wa Elimu na Mafunzo 53
SURA YA 6..........................................................................................55
6.0 MASUALA MTAMBUKO ....................................................................55
6.1 Utangulizi..........................................................................................55
6.2 Jinsia katika Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu na Mafunzo ..............55
6.3 Elimu ya Mazingira na Afya ya Jamii.................................................56
6.4 Ushauri na Unasihi katika Elimu na Mafunzo 59
6.5 Haki za Binadamu katika utoaji wa Elimu na Mafunzo 60
6.6 Haki za Mtoto katika Utoaji wa Elimu na Mafunzo 6590
6.7 Utawala Bora katika Mfumo wa Elimu na Mafunzo 61
SURA YA 7..........................................................................................61
7.0 MUUNDO WA KITAASISI ....................................................................61
7.1 Utangulizi..........................................................................................61
7.2 Ngazi ya Taifa ....................................................................................61
7.3 Ngazi ya Mkoa....................................................................................61
7.4 Halmashauri za Wilaya, Mji, Manispaa na Jiji .....................................61
7.5 Ngazi ya Kata .....................................................................................62
7.6 Ngazi ya Shule na Vyuo.......................................................................62

SURA YA 8..........................................................................................63
8.0 MUUNDO WA KISHERIA ....................................................................63
8.1 Sheria ya Kusimamia Elimu na Mafunzo 64
8.2 Vyombo vya Kisheria vya Kusimamia Elimu na Mafunzo .....................63
8.3 Sheria ya Kusimamia Shule na Vyuo vya Elimu na Mafunzo 64
SURA YA 9..........................................................................................65
9.0 HITIMISHO 64 Error! Bookmark not defined.

# DIBAJI

Elimu na mafunzo bora ni mkakati wa kipaumbele kufikia malengo ya mipango ya maendeleo yaliyowekwa. Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) pamoja na malengo ya Milenia vinaweka wazi umuhimu wa elimu na mafunzo katika kufikia malengo ya mipango hiyo.

Utoaji wa elimu na mafunzo bora unategemea sana sera zilizopo na utekelezaji wake. Sera ambazo zimekuwa zikitumika katika utoaji wa elimu na mafunzo ni Sera ya Elimu na Mafunzo 1995 Sera ya Taifa ya Elimu ya Juu 1999, Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo 1996. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa sera hizo, tathmini iliyofanyika mwaka 2008 ilionyesha kuwa kuna maeneo mengi ya sera hizo ambayo hayakutekelezwa ipasavyo kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo ukosefu wa fedha za kutosha na kutokuwa na muundo sahihi wa utekelezaji. Aidha, tathmini hiyo iliibua mahitaji mapya katika elimu na mafunzo yakiwemo uboreshaji wa mitaala, wajibu wa sekta isiyo rasmi katika elimu na mafunzo na umuhimu wa elimu ya ufundi na stadi za ujasiriamali.

Katika juhudi za kuinua ubora wa elimu na mafunzo hapa nchini, Serikali ililazimika kupitia upya Sera za Elimu na Mafunzo ili kukidhi mahitaji ya elimu na mafunzo hapa nchini.

Malengo ya Sera hii ni:

- Kuinua ubora wa elimu na mafunzo katika ngazi zote za elimu na mafunzo;
- Kuongeza uwezo wa asasi na taasisi za elimu na mafunzo kukidhi mahitaji yaliyopo;
- Kutoa elimu na mafunzo bora katika fani mbalimbali za elimu na mafunzo kukidhi mahitaji ya soko la ajira;
- Kuongeza wigo wa kuchangia kikamilifu gharama za elimu na mafunzo.
- Kutoa elimu kwa usawa kwa maeneo na makundi mbalimbali
- Kufanya tafiti za kielimu ili maamuzi yazingatie ushahidi wa kisayansi; na
- Kufanya ufuatiliaji na tathmini ili kujua mwenendo wa ufanisi na kufanya maamuzi rekebishi

inapobidi.

Ili kufikia malengo ya Sera hii kwa ukamilifu inahitaji ushirikiano wa wadau wote wa elimu na mafunzo katika ngazi zote wakiwemo sekta isiyo ya serikali, Asasi za Kiraia (AZAKI) na Washirika katika Maendeleo.

Mwisho, napenda kuwashukuru wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika mchakato mzima na kufanikisha kukamilisha Sera hii.

Dkt. Shukuru J. Kawambwa (Mb)

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi

SURA 1

## 1.0 UTANGULIZI

Elimu ni mjumuisho wa maarifa na stadi za kujitambua na kukabiliana na changamoto zilizopo katika mazingira na mabadiliko ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia. Elimu hupatikana kwa mchakato wa kufundisha na kujifunza. Mafunzo ni mchakato wa kupata maarifa, mwelekeo na stadi.

Utoaji wa elimu na mafunzo umekuwa ukiongozwa na sera za: Elimu na Mafunzo (1995); Elimu ya Ufundi na Mafunzo (1996); na Elimu ya Juu (1999). Aidha,utoaji wa elimu na mafunzo umekuwa ukiongozwa na sera za jumla za kitaifa, makubaliano na itifaki za kikanda na kimataifa. Utoaji wa elimu unazingatia maelekezo ya sera za jumla, kisekta, mikakati na programu mbalimbali za kitaifa; pamoja na masuala mtambuko.

Sera za Elimu na Mafunzo zilijikita zaidi katika kuelekeza uongezaji wa idadi ya wanafunzi shuleni na vyuoni kwa usawa na kukuza ubora wa elimu na mafunzo. Sera hizi pia zilisisitiza juu ya ushirikishwaji wa sekta binafsi na washirika wa maendeleo wa ndani na nje; hususan katika uanzishaji na uendeshaji wa shule na vyuo na ugharimiaji wa elimu na mafunzo. Vilevile, sera hizi zilisisitiza juu ya umuhimu wa kujenga utaifa; misingi ya maadili ya kitaifa; ushirikiano wa kitaifa na kimataifa; utawala wa sheria na kuzingatia Katiba ya nchi na matamko mengine muhimu ya kimataifa.

Katika kutekeleza sera za elimu na mafunzo, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu iliandaliwa mwaka 1997. Kutokana na programu hiyo, mipango mbalimbali iliandaliwa na kuanza kutekelezwa. Mipango hiyo ni: Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi Awamu ya Kwanza (MMEM I) 2002 – 2006; Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi Awamu ya Pili (MMEM II) 2007 - 2011; Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari Awamu ya Kwanza (MMES I)- 2004 – 2009; Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari Awamu ya Pili (MMES II) 2010 – 2015; na Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Juu (MMEJU) - 2010–2015. Aidha, Mpango wa

Maendeleo wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (MMEU) upo katika maandalizi. Mipango hii imezingatia malengo yaliyopo ya Dira ya Maendeleo ya Tanzania, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Elimu kwa Wote na Malengo ya Milenia.

Pamoja na jitihada za utekelezaji wa sera za elimu na mafunzo, upungufu ulijitokeza katika maeneo ya mfumo na muundo, uwezo katika uendeshaji, utawala na ugharimiaji. Aidha, kuna masuala ambayo hayakuwamo katika sera na mengine yameibuka kutokana na mabadiliko mbalimbali ya kitaifa na kimataifa yanayotakiwa kuzingatiwa. Sera za elimu na mafunzo zimepitiwa na kuhuishwa ili kupata sera ya elimu na mafunzo inayojitosheleza katika kukabiliana na changamoto zinazotokana na mabadiliko hayo.

## SURA YA 2

## 2.0 HALI YA UTOAJI WA ELIMU NA MAFUNZO NCHINI

### 2.1 Utoaji wa Elimu na Mafunzo Tangu Uhuru

Chimbuko la maendeleo ya elimu nchini ni matokeo ya michakato ya falsafa, sera na sheria zilizoanzishwa katika vipindi mbalimbali kabla na baada ya uhuru. Sera za ujumla za kijamii na kiuchumi zimejengeka tangu Uhuru wa Tanganyika ulipopatikana mwaka 1961. Baada ya uhuru, Serikali ilitunga Sheria ya Elimu Na. 83 ya mwaka 1962 iliyofuta Sheria ya Elimu ya mwaka 1927 ambayo iliruhusu utoaji wa elimu na mafunzo kwa mfumo wa ubaguzi wa rangi, dini na kabila. Katika Sheria Na. 83 ya mwaka 1962 Serikali ilielekeza kuwa mitaala, uongozi na ugharimiaji wa elimu na mafunzo ufuate usawa. Aidha, Kiswahili na Kiingereza zilifanywa kuwa lugha za kufundishia shuleni. Sheria Na. 50 ya mwaka 1969 iliweka utaratibu wa kuhamishia Serikalini vyuo vya ualimu na shule za mashirika binafsi na ya dini. Mwaka 1972 baadhi ya majukumu ya uendeshaji na usimamizi wa elimu yaliimarishwa chini ya Mpango wa Madaraka Mikoani.

Sheria mbalimbali muhimu zilitungwa ili kuimarisha utoaji wa elimu zikiwemo Sheria Na. 21 ya mwaka 1973 ya Baraza la Mitihani la Tanzania, Sheria Na. 12 ya mwaka 1975 ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Sheria Na. 13 ya mwaka 1975 ya Taasisi ya Elimu Tanzania, Sheria Na. 6 ya mwaka 1975 ya Bodi ya Huduma za Maktaba; Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 inayosimamia elimu na mafunzo na Sheria Na. 1 ya mwaka 1994 ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

Tamko la Azimio la Arusha la mwaka 1967 ni chimbuko la falsafa ya Ujamaa na Kujitegemea ambayo ilisababisha mabadiliko makubwa katika sera za jumla za kijamii na kiuchumi. Azimio la Musoma 1974 liliweka mkazo kuhusu Elimu ya Msingi kwa Wote, uchangiaji wa elimu ya juu na kufanya kazi kabla ya kujiunga na chuo kikuu, isipokuwa kwa wasichana ambao waliruhusiwa kujiunga moja kwa moja. Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea ilijikita katika:

- kuondoa matabaka katika utoaji elimu na kuwafanya wanafunzi kuthamini kazi za mikono na kuoanisha waliyojifunza darasani na shughuli za jamii;

- kuondoa utengano kati ya shule na jamii na kusaidia kuondoa kasumba ya wasomi ya kujibagua na kutotumia elimu waliyoipata kwa maendeleo ya jamii;.
- kuoanisha nadharia na vitendo, ili elimu isipatikane vitabuni tu, bali ijumuishe ile ipatikanayo kutokana na uzoefu wa kutenda au kufanya kazi za kuongeza tija;
- kuzifanya shule na vyuo kuwa vituo vya uzalishaji mali ili kuchangia gharama za uendeshaji; na
- kuifanya elimu inayotolewa katika kila ngazi imwezeshe mhitimu kuishi na kufanya kazi yenye manufaa katika jamii.

Pamoja na umuhimu wa falsafa ya Elimu ya Kujitegemea, utoaji wa elimu na mafunzo uliegemea zaidi kwenye taaluma inayolenga utoaji wa maarifa na stadi kwa nadharia bila kuzingatia vitendo. Kuanzia mwaka 1995, utoaji wa elimu na mafunzo nchini uliongozwa na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya mwaka 1996 na Sera ya Taifa ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999. Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 ulipata nguvu kutokana na marekebisho ya Sheria Na. 10 ya mwaka 1995 ya Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. .

Katika jitihada za kuimarisha elimu nchini, vyombo mbalimbali viliundwa kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa sera za elimu na mafunzo. Vyombo hivyo ni pamoja na: Chuo cha Uongozi na Usimamizi wa Elimu ambacho sasa kimekuwa Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (Agency for Development of Educational Management – ADEM Act 2001), Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (Tanzania Comission for Universities-TCU, Universities Act 2005); Mamlaka ya Elimu Tanzania (Tanzania Education Authority – TEA - The Education Fund Act 2001); Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (Higher Education Students’ Loans Board – HESLB Act 2004) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (National Council for Technical Education – NACTE Act No. 9 of 1997).

Sera ya Elimu na Mafunzo na sera nyingine za elimu zimekuwa zikitekelezwa kwa

kuzingatia falsafa ya elimu ya kujitegemea na sera za jumla za taifa ambazo ni Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 (Tanzania Development Vision 2025) ya mwaka 1999 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA) wa mwaka 2005. Ili kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo (1995), Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (Education Sector Development Programme - ESDP) ilianzishwa mwaka 1997 kwa lengo la kujumuisha mipango ya sekta ndogo za elimu kwa mfumo jumuishi badala ya kila sekta ndogo ya elimu kuwa na mpango wake. Kutokana na Programu hii, Mipango ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), Sekondari (MMES) na Mpango ya Maendeleo ya Elimu ya Juu (MMEJU) iliandaliwa na kutekelezwa. Aidha, Mpango wa Elimu ya Ufundi (MMEU) upo katika hatua za maandalizi.

## 2.2. Mfumo na Muundo wa Elimu na Mafunzo

Mfumo wa Elimu na Mafunzo wa Tanzania una mpangilio wa ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo. Mfumo huu una sehemu kuu mbili, mfumo wa muda maalum na mfumo huria.

Mfumo wa muda maalum wa elimu na mafunzo ni wa kitaaluma na kitaalamu ukianzia ngazi ya elimu ya msingi hadi elimu ya juu. Muundo wa elimu na mafunzo wa kitaaluma unaotumika ni 2-7-4-2-3+: ambapo miaka 2 ya Elimu ya Awali, miaka 7 ni ya Elimu ya Msingi; miaka 4 ni ya Elimu ya Sekondari ya ngazi ya Kawaida; miaka 2 ni ya Elimu ya Sekondari ya Ngazi ya Juu; na miaka 3 au zaidi ni ya Elimu ya Juu. Muundo wa elimu na mafunzo wa kitaalamu unaanza baada ya elimu ya sekondari na inakuwa ya mwaka mmoja (1) au zaidi na kuendelea mpaka elimu ya juu.

Elimu na mafunzo nchini Tanzania husimamiwa na wizara yenye dhamana ya elimu na mafunzo. Wizara nyingine, taasisi na idara za Serikali na zisizo za Serikali ni washiriki katika utoaji wa elimu na mafunzo kwa mfumo rasmi na usio rasmi.

### a) Elimu ya Awali

Serikali inatambua kuwa Elimu ya Awali ni muhimu kwa maendeleo ya mtoto kimwili, kiakili na kimaadili. Utafiti kadhaa uliofanyika nchini katika miaka ya 1980 umelibaini kuwa watoto waliopitia elimu ya awali huwa na mafanikio makubwa zaidi wanapoanza darasa la kwanza.
Kutokana na kutambua umuhimu huu, Serikali iliamua kuingiza Elimu ya Awali kwa

watoto wenye umri wa miaka 5 na 6 kwenye mfumo rasmi wa elimu na kila shule ya msingi inapaswa kuwa na madarasa ya Elimu ya Awali. Baadhi ya watoto wadogo wenye umri chini ya miaka 5 wanalelewa na kupewa elimu katika vituo vya kulelea watoto wadogo.

### b) Elimu ya Msingi

Elimu ya Msingi inatolewa kwa miaka saba (7) na ni ya lazima kwa uandikishaji na mahudhurio kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Baada ya Elimu ya Msingi, baadhi ya wahitimu huendelea na Elimu ya Sekondari, Mafunzo ya Ufundi Stadi; na waliokosa fursa hizo huingia kwenye ulimwengu wa kazi. Elimu ya msingi inatekelezwa kwa kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi.

### c) Elimu ya Sekondari

Elimu ya Sekondari inatolewa kwa miaka 6. Elimu hii imegawanyika katika Ngazi ya Kawaida ya miaka minne ya Kidato cha 1 hadi 4; na Ngazi ya Juu ya miaka miwili ya Kidato cha 5 na 6. Wanafunzi wanaohitimu Elimu ya Sekondari Ngazi ya Kawaida huendelea kwenye Elimu ya Sekondari Ngazi ya Juu; mafunzo ya Kitaalamu; na ulimwengu wa ajira. Waliohitimu Elimu ya Sekondari Ngazi ya Juu hujiunga na taasisi na vyuo vya Elimu ya Juu; na soko la ajira. Elimu ya Sekondari inatekelezwa kwa kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari.

### d) Elimu ya Ualimu

Elimu ya Ualimu inatolewa katika Vyuo vya Ualimu na Vyuo Vikuu vya Serikali na visivyo vya Serikali. Vyuo vya Ualimu vinatoa mafunzo ya Cheti Daraja A kwa Walimu wa shule za Msingi na Stashahada kwa Walimu wa shule za Sekondari Ngazi ya Kawaida. Elimu ya Ualimu ngazi ya cheti inatolewa kwa wahitimu wa Elimu ya Sekondari ngazi ya kawaida na ya stashahada kwa wahitimu wa Elimu ya Sekondari ngazi ya juu. Vyuo Vikuu vinatoa Walimu kwa ajili ya shule za Sekondari Ngazi ya Juu na Wakufunzi kwa ajili ya Vyuo vya Ualimu. Elimu ya Ualimu inatekelezwa kwa kutumia Mkakati wa Maendeleo na Menejimenti ya Walimu.

### e) Elimu ya Ufundi na Mafunzo

Elimu ya Ufundi na Mafunzo inaambatana na upataji wa maarifa na stadi kwa ajili ya ajira au kujiendeleza zaidi kiufundi na kitaalamu. Elimu hii ina programu za biashara, ufundi na mafunzo ya kazi yanayoendeshwa na wizara mbalimbali, mashirika yasiyo ya Kiserikali na taasisi binafsi. Elimu ya Ufundi na Mafunzo

hutolewa katika ngazi ya cheti, stashahada na shahada. Elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ngazi ya cheti hutolewa na vyuo vinavyosimamiwa na kuratibiwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Elimu ya Ufundi na mafunzo ngazi ya cheti, stashahada na shahada hutolewa na vyuo vya wizara za sekta husika pamoja na taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Serikali. Elimu na mafunzo haya ni muhimu kwa kutoa rasilimaliwatu inayotumika viwandani, mashambani na katika sekta nyingine za uzalishaji na huduma. Ngazi ya cheti inachukua wanafunzi wanaohitimu Elimu ya Msingi na ya Sekondari. Ngazi ya stashahada inachukua wanafunzi waliohitimu elimu ya Sekondari na baadhi ya wahitimu wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ngazi ya cheti. Ngazi ya shahada inachukua wahitimu wa elimu ya sekondari ya juu na baadhi ya wahitimu wa elimu ya ufundi na mafunzo ngazi ya stashahada. Elimu ya ufundi katika ngazi ya cheti, stashahada na shahada inaratibiwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi

f) Elimu ya Juu.

Elimu ya Juu ni elimu itolewayo baada ya Elimu ya Sekondari na hutolewa katika vyuo vya Serikali na visivyo vya Serikali. Taasisi za elimu ya juu hutoa mafunzo ya kitaalamu na hutuza vyeti, stashahada, shahada, stashahada za uzamili, shahada za uzamili na uzamivu. Taasisi hizi zina wajibu wa kufundisha, kufanya utafiti, kutoa ushauri wa kitaalamu na kuandaa na kutoa kada za wataalamu wa ngazi ya kati na ngazi ya juu. Katika kuinua ubora na kupanua Elimu ya Juu, vyombo mbalimbali vilianzishwa kwa nyakati tofauti ikiwa ni pamoja na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania; Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi; Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na Mamlaka ya Elimu Tanzania.

g) Elimu Nje ya Mfumo Rasmi

Elimu na Mafunzo nje ya mfumo rasmi ni utaratibu wa utoaji wa elimu kwa watu ambao hawakupata fursa ya elimu na mafunzo katika mfumo wa kawaida. Elimu na Mafunzo inayotolewa kwa utaratibu huu, hujumuisha Kusoma, Kuandika, Kuhesabu (KKK) na kujiendeleza kwa lengo la kupata maarifa na stadi mbalimbali za kazi na za maisha. Elimu na Mafunzo ya aina hii hutolewa kwa njia ya masafa, huria na ana kwa ana. Elimu inayotolewa kwa utaratibu huu ni pamoja na ile inayotolewa kupitia Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii (MUKEJA) ambao

hutoa elimu na mafunzo kwa watu wazima kwa ajili ya kuwawezesha kufanya kazi zao katika jamii kwa tija na ufanisi. Aidha, watoto wenye umri wa miaka 11 – 18 waliokosa Elimu ya msingi kupitia mfumo rasmi huipata elimu hiyo kupitia Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Watoto Walioikosa (MEMKWA).

#### h) Ugharimiaji wa Elimu na Mafunzo

Serikali kuu kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa hugharimia elimu na mafunzo. Aidha, wazazi, jamii na washirika wa maendeleo wa elimu na mafunzo hushiriki katika kugharimia elimu na mafunzo. Katika juhudi za kuongeza tija na ufanisi, mifuko mbalimbali ilianzishwa. Mifuko hiyo ni pamoja na Mfuko wa Elimu - mwaka 2001, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na kodi ya maendeleo ya stadi ya mwaka 1994.

## 2.3 Mafanikio

Katika kutekeleza sera za elimu na mafunzo kumekuwepo na mafanikio mbalimbali kama ifuatavyo:

- kurasimishwa kwa elimu ya awali kwa watoto wenye umri wa miaka 5 hadi 6;
- kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi katika ngazi zote za elimu na mafunzo;
- kuimarika kwa uwiano kati ya wavulana na wasichana katika ngazi zote za elimu na mafunzo;
- kuimarika kwa uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi katika ngazi zote za elimu na mafunzo;
- kuongezeka kwa idadi ya vyuo vya elimu ya juu nchini;
- kuanzishwa kwa vyombo mbalimbali vya kudhibiti ubora wa elimu na mafunzo;
- kupanuliwa kwa wigo wa ugharamiaji wa elimu na mafunzo nchini;
- kuimarika kwa ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa elimu na mafunzo; na
- kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia katika utoaji wa elimu na mafunzo.

## 2.4 Changamoto

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, umejitokeza upungufu katika mfumo na muundo na utekelezaji katika maeneo ya: uendeshaji; utawala, usimamizi na

ugharimiaji; mawasiliano ndani ya Wizara; na mawasiliano ya kitaasisi. Hali kadhalika, upungufu wa rasilimaliwatu, fedha na vifaa na katika sheria mbalimbali zilizoanzisha vyombo vya elimu umechangia katika kudhoofisha utekelezaji wa sera za elimu na mafunzo nchini. Baadhi ya changamoto hizo ni:-

- idadi ndogo ya watoto wanaandikishwa katika elimu ya awali;
- uandikishwaji mdogo wa wanafunzi katika maeneo yenye mazingira magumu;
- uwiano usioridhisha wa mwalimu kwa wanafunzi katika ngazi ya sekondari;
- kutokuwepo kwa mwamko wa kutosha katika jamii kuhusu umuhimu wa elimu na mafunzo kwa watoto wa kike na wenye ulemavu;
- mdondoko wa wanafunzi shuleni;
- mitaala na programu za elimu na mafunzo zisizokidhi mahitaji ya jamii na soko la ajira;
- uwezo mdogo wa baadhi ya watendaji katika mfumo wa usimamizi na uendeshaji wa elimu na mafunzo;
- ukosefu wa uratibu thabiti wa wizara na taasisi mbalimbali zinazotoa elimu na mafunzo;
- tija na ufanisi mdogo katika mfumo wa utekelezaji wa sera za elimu na mafunzo;
- ufinyu wa nafasi za elimu ya juu nchini;
- upungufu wa walimu wa sayansi, hisabati, teknolojia na lugha;
- walimu kuacha kazi na wengine kutopenda kufanya kazi katika maeneo yenye mazingira magumu;
- upungufu, uchakavu wa mitambo, mashine na vifaa vilivyopitwa na wakati; na uchakavu wa miundombinu katika taasisi za elimu na mafunzo;
- upungufu wa rasilimaliwatu katika kada mbalimbali za elimu na mafunzo;
- fursa finyu za mfumo wa elimu na mafunzo zisizotoa fursa anuwai za elimu na mafunzo; na
- kuongezeka kwa idadi ya vijana na watu wazima wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu.

SURA 3

# 3.0 UMUHIMU WA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO

## *3.1* Usuli

Sera ni matamko yatokanayo na masuala ya msingi yenye dhamira ya kuelekeza namna ya kukabili changamoto kwa ajili ya maendeleo katika jamii. Aidha, inaweka wazi dira na dhima na kuelekeza juu ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara, idara, taasisi, sekta binafsi na jamii kwa ujumla. Sera inazingatia Dira ya Taifa na mikakati ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa. Wananchi ndiyo chimbuko, walengwa wakuu, wadau na watekelezaji wa sera.

Sera za Elimu na Mafunzo (1995), Elimu ya Ufundi na Mafunzo (1996) na Elimu ya Juu (1999) zimekuwa zikitumika kwa kipindi cha zaidi ya muongo mmoja. Sera hizo zimetafsiriwa katika mipango mbalimbali ya utekelezaji. Baadhi ya mipango hiyo ni Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu, Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi ,Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari na Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Juu . Mipango hiyo imeandaliwa kwa kuzingatia maelekezo ya sera na mikakati ya jumla ya kitaifa na kimataifa kama vile; Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania, Elimu kwa Wote na Malengo ya Maendeleo ya Milenia.

## *3.2* Mabadiliko Yaliyojitokeza katika Utekelezaji wa Sera za Elimu na Mafunzo.

Tangu kuanza kutekelezwa kwa Sera za Elimu na Mafunzo, kumekuwa na mabadiliko mbalimbali ya kisiasa, kijamii, kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia ambayo yanaleta changamoto katika mipango ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo. Aidha, kuna masuala ambayo yameibuka kutokana na mabadiliko mbalimbali ya kitaifa na kimataifa na kushawishi kupitiwa kwa sera na mikakati mbalimbali ya Elimu na Mafunzo. Masuala hayo ni pamoja na Utandawazi, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Elimu ya Jinsia, Utawala Bora, Stadi za Maisha, Ushauri na Unasihi, Huduma na faraja kwa wanaoishi na Virusi vya

UKIMWI (VVU) na wenye UKIMWI, Elimu Jumuishi na Elimu ya Mazingira na Afya ya Jamii.

Matamko ya kitaifa, kimataifa na kikanda ambayo yamezingatiwa katika uhuishaji wa Sera za Elimu na Mafunzo ni pamoja na:

i) Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 ya mwaka 2000 inayolenga kuwa na jamii iliyoelimika na yenye utayari wa kuendelea kujifunza;
ii) Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (2005 na 2010) unaosisitiza kuinua ubora wa maisha kwa kuimarisha uwezo wa rasilimaliwatu;
iii) Itifaki ya SADC kuhusu elimu na mafunzo – (Blantyre 1997) inayosisitiza kuimarisha ushirikiano katika maeneo mbalimbali ya elimu na mafunzo kwa nchi wanachama;
iv) Elimu kwa Wote (Dakar Framework of Action 2000) ambayo inasisitiza haki ya elimu bora kwa watoto wote na watu wazima bila kujali tofauti zao na kuwajumuisha watoto wenye ulemavu kwenye madarasa ya kawaida;
v) Malengo ya Maendeleo ya Milenia ambayo pamoja na kusisitiza ulazima wa kuwa na elimu bora ya msingi kwa wote yanaelekeza juu ya upatikanaji wa elimu ya mazingira na ya kujikinga na maambukizi ya VVU;
vi) UNESCO_PERTH Declaration, 2007 kuhusu utoaji wa elimu ya Sayansi na Teknolojia inayokidhi mahitaji na yenye tija katika ngazi zote za elimu na mafunzo;
vii) makubaliano katika mkutano mkuu wa UNESCO karne ya 21 (Paris 2002) kuhusu kuimarisha utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo katika mfumo wa elimu na mafunzo; na
viii) makubaliano ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Elimu na Mafunzo yanatamka kwamba kila nchi mwanachama itachukua hatua madhubuti za kuimarisha ushirikiano katika maeneo mbalimbali ya elimu na mafunzo.

Mabadiliko na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa sera za elimu na mafunzo, sera za jumla za taifa na makubaliano ya kimataifa kuhusu elimu na mafunzo, yamekuwa chimbuko la kupitia sera za elimu na mafunzo ili kupata sera inayokidhi mahitaji.

## SURA 4

## 4.0 FALSAFA, DIRA, DHIMA NA MADHUMUNI YA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO

### *4.1* Falsafa

Elimu inayotolewa nchini inazingatia misingi ya Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea ya mwaka 1967. Misingi hiyo ni ujifunzaji wenye manufaa katika nyanja zote kuu tatu: utambuzi, utendaji na mwelekeo. Ujifunzaji wa aina hii unatambulishwa na viashiria ambavyo ni pamoja na: ushirikishaji, uhusishaji wa nadharia na vitendo, uadilifu, kujiamini, kujiendeleza, kuwa na stadi za maisha, ushindani, kuthamini usawa, ujasiriamali, ubunifu, udadisi, uvumbuzi, uwezo wa kuchambua na kutathmini.

Utoaji wa elimu na mafunzo nchini utaendelea kuzingatia misingi ya Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea na mabadiliko yanayotokea katika jamii kisiasa, kiutamaduni, kiuchumi na kiteknolojia.

### *4.2* Dira

Sera ya elimu na mafunzo inadhamiria kuwa na:
"Mtanzania aliyeelimika kwa kiwango cha juu, mwenye maarifa, stadi na mwelekeo; mahiri na aliye tayari kukabiliana na changamoto za kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiteknolojia; na kushiriki kwa ufanisi katika kufikia malengo ya maendeleo yaliyowekwa kitaifa na kimataifa".

### *4.3* Dhima

Kutoa fursa ya elimu na mafunzo bora kwa usawa na kuhakikisha kuwepo kwa mazingira yanayokidhi mahitaji kiutendaji kwa wadau wote wa elimu na mafunzo ili waweze kushiriki katika kutoa elimu hiyo katika ngazi zote.

## *4.4* Madhumuni

### 4.4.1. Madhumuni ya Jumla

Kuelekeza juu ya utoaji wa elimu na mafunzo unaozingatia mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiteknolojia pamoja na mahitaji ya soko la ajira, ili kuinua ubora wa maisha ya Mtanzania.

### 4.4.2. Madhumuni Mahsusi

Sera ya elimu na mafunzo ina madhumuni mahsusi yafuatayo:

a) Kuweka mfumo na muundo wa elimu na mafunzo unaotoa fursa kwa usawa wa kijinsia na kwa makundi mbalimbali yakiwemo ya watu wenye ulemavu, wenye vipaji na vipawa tofauti.

b) Kuandaa na kuendeleza rasilimaliwatu katika viwango mbalimbali vitakavyokidhi mahitaji ya jamii.

c) Kushirikisha taasisi na asasi za Serikali na zisizo za serikali, watu binafsi na washiriki wa maendeleo katika utoaji wa elimu na mafunzo.

d) kuandaa mitaala inayozingatia nadharia na vitendo katika nyanja zote za elimu na Mafunzo.

e) Kupanua wigo wa ugharimiaji wa elimu katika ngazi zote za elimu na mafunzo kwa kushirikisha wadau wote.

f) kutoa elimu ya mazingira katika ngazi zote za elimu na mafunzo;

g) kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa elimu na mafunzo kati ya nchi wanachama kikanda na kimataifa;

h) Kujenga uwezo wa jamii ya wanafunzi na wafanyakazi wa sekta ya elimu na mafunzo katika kujikinga na maradhi na matumizi mabaya ya dawa za kulevya, na kutoa huduma na faraja;

i) Kupanua upeo wa maarifa na kujenga stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu na kujenga utamaduni wa kuendelea kujielimisha;

j) kuimarisha uratibu na usimamizi wa utoaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote za elimu;

k) kuweka muunganiko na mlinganisho kati ya ngazi za elimu na mafunzo unaoruhusu uhuru wa mwingiliano wa kupata sifa stahiki katika ngazi mbalimbali; na

l) kutumia TEHAMA katika elimu na mafunzo ili kuleta ufanisi katika utoaji wa elimu na mafunzo.

SURA YA 5

# 5.0 HOJA ZA SERA NA MATAMKO

## *5.1* Mfumo wa Elimu na Mafunzo

Mfumo wa Elimu na Mafunzo ni utaratibu wa utoaji wa elimu na mafunzo. Utoaji huo wa elimu na mafunzo hufanyika kwa utaratibu wa muda maalumu na huria.

Utaratibu wa muda maalumu unampa nafasi mlengwa kujifunza katika sehemu iliyoainishwa na kuzingatia muda maalumu wa kuhitimu ngazi moja ya elimu. Utaratibu huria unampa mlengwa nafasi ya kuchagua programu anayopenda, kujifunza mahali popote na kwa njia yoyote kulingana na kasi na uwezo wa mhusika.

### Suala

Ufanisi wa mfumo wa elimu na mafunzo

### Maelezo

Mfumo wa elimu na mafunzo uliopo hauna ufanisi na tija inayotarajiwa. Aidha uratibu wa wizara na taasisi zinazohusika na usimamizi na utoaji wa elimu na mafunzo haukidhi mahitaji na matarajio ya jamii.

Kuna umuhimu wa kurekebisha mfumo na kuimarisha uratibu wa utoaji na usimamizi wa elimu na mafunzo.

### Madhumuni

Kuwa na mfumo wa elimu wenye tija na ufanisi

### Tamko

*5.1.1 Serikali itaimarisha mfumo wa elimu na mafunzo ili kuleta tija na ufanisi.*

*5.1.2 Serikali itaimarisha uratibu wa utoaji wa elimu baina ya wizara na taasisi za elimu na mafunzo ili kuongeza tija na ufanisi katika mfumo wa elimu.*

## *5.2* Muundo wa Elimu na Mafunzo

Muundo wa elimu na mafunzo ni mpangilio wa utoaji wa elimu na mafunzo katika ngazi na programu mbalimbali ili kuweka msingi wa kuandaa na kuendeleza rasilimaliwatu katika viwango mbalimbali vitakavyokidhi mahitaji ya jamii.

### Suala

Muundo stahiki wa elimu na mafunzo

### Maelezo

Muundo wa elimu uliopo wa 2-7-4-2-3+ humchukua mwanafunzi jumla ya miaka kumi na nane kuukamilisha na hivyo kuchelewa kutoa mchango wake kwa taifa. Elimu ya msingi kwa sasa ni ya lazima na ni haki ya kila mtoto. Mhitimu wa elimu hii anakuwa na umri mdogo, na maarifa yasiyotosheleza kujiunga na mafunzo ya kazi au kukabiliana na changamoto za ulimwengu wa kazi. Elimu ya sekondari inamwandaa mhitimu kujiunga na mafunzo ya kazi na elimu ya juu.

Ili kupata mhitimu mwenye umri na kiwango cha elimu cha kutosha kumwingiza katika mafunzo ya kazi na ulimwengu wa kazi, kuna umuhimu wa kutoa ‘elimu–msingi’ ya miaka 11 itakayojumuisha elimu ya awali, msingi na sekondari kawaida.

### Madhumuni

Kuwa na muundo fanisi na wenye tija katika utoaji wa elimu na mafunzo.

### Tamko

*5.2.1 Elimu ya Msingi na Sekondari ngazi ya kawaida itakuwa Elimu-Msingi na itakuwa ya lazima*

*5.2.2 Muundo wa elimu na mafunzo wa kitaaluma utakuwa 1-6-4-2-3+ yaani, mwaka mmoja wa elimu ya awali, miaka 6 ya elimu*

*ya msingi, miaka 4 ya elimu ya sekondari ya kawaida, miaka 2 ya elimu ya sekondari ya juu na miaka isiyopungua 3 ya elimu ya juu.*

*5.2.3 Muundo wa elimu na mafunzo wa kitaalamu utakuwa 1-6-4-1+ yaani, mwaka mmoja wa elimu ya awali, miaka 6 ya elimu ya msingi, miaka 4 ya elimu ya sekondari ya kawaida, mwaka 1 au zaidi wa elimu ya ufundi na mafunzo.*

*5.2.4 Muundo wa elimu na mafunzo utamwezesha mwanafunzi kutoka muundo mmoja kwenda mwingine.*

### Elimu katika Vituo vya Kulelea Watoto Wadogo

Elimu katika vituo vya kulelea watoto wadogo hutolewa kwa watoto wenye umri chini ya miaka 5. Watoto hawa wanahitaji mazingira rafiki yatakayowawezesha kuwa na maendeleo bora kimwili, kiakili na mwelekeo na kuendelea kujifunza kwa ufanisi.

#### Suala

Mazingira ya kutolea Elimu katika vituo vya kulelea watoto wadogo.

#### Maelezo

Elimu imekuwa ikitolewa kwa watoto wenye umri chini ya miaka 5 katika vituo vya watoto wadogo bila uratibu thabiti. Katika vituo vingi, elimu hiyo imekuwa ikitolewa katika mazingira yasiyozingatia misingi bora ya elimu. Aidha, elimu hiyo imekuwa ikitolewa pasipo vituo husika kutambuliwa rasmi na kuratibiwa. Mtoto anahitaji malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto chini ya uangalizi wa mzazi au mlezi. Hivyo, vituo vya kulelea watoto wadogo viwe vya kutwa tu isipokuwa kwa watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi. Ili kuwezesha utoaji wa elimu bora yenye muunganiko na ngazi nyingine za elimu, vituo vya kulelea watoto wadogo havina budi kutambuliwa rasmi na kuratibiwa.

#### Madhumuni

Kuwa na msingi imara wa elimu na mafunzo kwa watoto wadogo.

Tamko

*5.2.5 Serikali itahakikisha kuwa vituo vya kulelea watoto wadogo vinatambuliwa rasmi na kuratibiwa.*

*5.2.6 Serikali itahakikisha kuwa watoto walioko katika vituo vya kulelea watoto wadogo wanapewa huduma stahiki na elimu bora.*

*5.2.7 Serikali itahakikisha kuwa watoto wenye ulemavu, vipaji, vipawa na mahitaji mengine maalumu katika vituo vya kulelea watoto wadogo wanapata huduma stahiki na kuendelezwa katika elimu na mafunzo.*

*5.2.8 Serikali itahakikisha kuwa Vituo vya kulelea watoto wadogo ni vya kutwa isipokuwa makao ya watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi.*

Elimu ya Awali

Elimu ya awali ni elimu inayomwandaa mtoto kwa ajili ya elimu ya Msingi.

Suala

Utoaji wa Elimu ya Awali.

Maelezo

Elimu ya Awali imekuwa ikitolewa kwa watoto wenye umri wa miaka mitano kwa muda wa miaka miwili. Uzoefu unaonesha kuwa elimu hii inaweza kutolewa kwa muda wa mwaka mmoja ikiwa programu za elimu hii zimeandaliwa na kutolewa kwa ufanisi. Aidha, mtoto wa miaka sita ana utayari wa kuanza elimu ya msingi.

Madhumuni

Kuwa na muundo fanisi katika utoaji wa Elimu ya Awali.

Tamko

*5.2.9 Elimu ya Awali itatolewa kwa watoto wenye umri wa miaka mitano kwa kipindi cha mwaka mmoja.*

*5.2.10 Serikali itahakikisha kuwa watoto walioko kwenye madarasa ya elimu ya awali wanasoma kwa utaratibu wa kutwa na wanapata huduma muhimu .*

*5.2.11 Serikali itahakikisha kuwa watoto wenye ulemavu, vipaji, vipawa na mahitaji mengine maalumu katika madarasa ya Elimu ya Awali wanapata huduma stahiki na kuendelezwa katika elimu na mafunzo.*

Elimu ya Msingi

Elimu ya msingi inakusudiwa kumwezesha kila mtoto kupata maarifa, mwelekeo, ujuzi na stadi za msingi za kusoma, kuandika, kuhesabu, kubaini na kutambua changamoto zilizopo katika mazingira na mbinu za kukabiliana nazo.

Suala

Utoaji wa Elimu ya Msingi kwa wote.

Maelezo

Madhumuni makuu ya Elimu ya Msingi ni kumpa mtoto elimu na mafunzo bora yatakayokuwa msingi wa elimu na mafunzo na kumuandaa kukabiliana na changamoto mbalimbali katika jamii. Umri wa kuanza elimu ya msingi umekuwa ni miaka saba. Katika umri huu mtoto anakuwa amechelewa kuanza kupata elimu ya msingi, na hivyo kuingia kwenye umri wenye vishawishi vingi ambavyo vinaweza kusababisha kutoandikishwa shule au kukatisha masomo. Aidha, kwa kuwa uzoefu unaonesha kuwa mtoto wa umri wa miaka sita anamudu elimu ya msingi, kuna umuhimu wa kupunguza umri wa kuanza elimu hiyo ili kuongeza ufanisi katika mfumo mzima wa elimu.

### Madhumuni

Kutoa Elimu ya Msingi kwa wote na kwa ufanisi.

### Tamko

*5.2.12 Elimu ya Msingi itakuwa ni haki kwa wote; na ya lazima kwa watoto wote waliofikia umri wa miaka sita*

*5.2.13 Serikali itahakikisha kuwa watoto wote wenye umri wa miaka sita wanapata Elimu ya Msingi kwa miaka sita.*

### Suala

Kuendeleza watoto wenye mahitaji maalumu

### Maelezo

Mfumo wa elimu uliopo unatoa nafasi ya mtoto kupata elimu ya awali, msingi na sekondari kwa ujumla bila kuzingatia mahitaji na vipaji alivyo navyo. Utaratibu uliopo hautoi fursa ya kubaini, kukuza na kuendeleza vipaji vya watoto katika umri mdogo na badala yake huwafikiria wale wenye ufaulu wa juu wa mitihani kuwa ndio pekee wenye vipaji. Aidha, hakuna utaratibu wa kuwabaini na kuwawezesha wanafunzi wenye ulemavu na wenye matatizo ya kujifunza kupata elimu stahiki. Hali hii haitoi fursa ya kubaini, kukuza na kuendeleza vipaji vya watoto katika umri mdogo na hivyo kupoteza rasilimaliwatu muhimu kwa maendeleo ya taifa. Kuna umuhimu wa kubaini na kuwaendeleza watoto wote kulingana na mahitaji yao.

### Madhumuni

Kuwaendeleza watoto wenye mahitaji maalumu kulingana na mahitaji yao.

### Tamko

5.2.14 *Serikali itahakikisha kuwa watoto wenye ulemavu, vipaji, vipawa na mahitaji mengine maalumu katika madarasa ya Elimu ya Msingi wanapata huduma stahiki na kuendelezwa katika elimu na mafunzo kulingana na uwezo wao.*

### Elimu ya Sekondari

Elimu ya sekondari hutolewa kwa wanafunzi ambao wamehitimu elimu ya msingi. Elimu hii ina ngazi mbili: elimu ya sekondari ya kawaida ya miaka minne; na elimu ya sekondari ya juu ya miaka miwili. Madhumuni makuu ya elimu ya sekondari ni kutoa nafasi ya kupata maarifa, stadi na mwelekeo ili wahitimu wajiunge na mafunzo ya elimu ya juu na ulimwengu wa ajira.

#### Suala

Ubora wa elimu ya sekondari.

#### Maelezo

Kupanuka kwa sekta rasmi na isiyo rasmi kumeongeza shughuli za kiuchumi zinazohitaji rasilimaliwatu yenye maarifa, stadi na mwelekeo stahiki. Utoaji wa elimu ya sekondari umejikita zaidi katika nadharia kuliko vitendo. Mahitaji ya sasa na yajayo ya rasilimaliwatu yanahitaji wahitimu wenye mwelekeo na umahiri katika stadi za fani mbalimbali. Kwa hiyo, elimu ya sekondari haina budi kutayarisha rasilimaliwatu itakayokidhi mahitaji hayo.

#### Madhumuni

Kutoa elimu ya sekondari itakayomwezesha mhitimu kupata maarifa, mwelekeo na stadi za maisha zinazokidhi mahitaji.

#### Tamko

5.2.15 *Serikali itaimarisha utoaji wa elimu ya sekondari ili kuwezesha wanafunzi kupata maarifa na stadi mbalimbali katika ngazi hii ya elimu na mafunzo.*

5.2.16 *Serikali itahakikisha kuwa wanafunzi wanaosajiliwa katika*

*elimu ya sekondari wanakamilisha mzunguko huo wa elimu.*

*5.2.17 Serikali itahakikisha kuwa watoto wenye ulemavu, vipaji, vipawa na mahitaji mengine maalumu katika Elimu ya sekondari wanapata huduma stahiki na kuendelezwa.*

### Elimu ya Ualimu

Elimu ya ualimu ni maarifa, stadi na mwelekeo unaomwezesha mhitimu kuelimisha na kufundisha. Elimu hiyo hutolewa katika vyuo vya ualimu na vyuo vikuu.

#### Suala

Ubora wa elimu ya ualimu

#### Maelezo

Programu za elimu ya ualimu zinazotolewa katika ngazi za cheti, stashahada na shahada hazina muunganiko wa kimaudhui kutoka ngazi moja kwenda nyingine. Baadhi ya wakufunzi hawana taaluma ya ualimu na wengine hawana uzoefu wa kufundisha katika ngazi yoyote ya elimu. Walimu wanafunzi wanamaliza mafunzo ya ualimu bila kuwa na mazoezi ya vitendo yenye kutosheleza mahitaji. Mazoezi ya vitendo ni muhimu kwa ajili ya kuwapa wanachuo uzoefu wa kufundisha na kukabiliana na changamoto zilizopo katika mazingira halisi watakayofanyia kazi baada ya kuhitimu. Mafunzo ya walimu kazini humwezesha mwalimu kuoanisha mafunzo ya awali na mahitaji halisi ya kazi ya ualimu. Aidha, taaluma ya ualimu haina mamlaka ya kusimamia utambuzi, usajili na maadili ya ualimu baada ya kuhitimu. Ni muhimu kuwa na mafunzo ya msingi ya elimu ya ualimu na ya kujiendeleza kitaalamu, na udhibiti wa taaluma hiyo.

#### Madhumuni

Kuwa na elimu ya ualimu inayokidhi mahitaji.

#### Tamko

*5.2.18 Serikali itaimarisha utoaji wa elimu ya ualimu kwa kuwa na*

*mafunzo ya msingi ya elimu ya ualimu yenye muunganiko wa kitaalamu kwa ngazi zote.*

*5.2.19 Utoaji wa elimu ya ualimu utazingatia mahitaji na vipaumbele vya taifa.*

*5.2.20 Mafunzo kabilishi na rejeshi kwa walimu yatakuwa ya lazima.*

*5.2.21 Vituo vya kuwaendeleza walimu vitaimarishwa katika ngazi mbalimbali.*

*5.2.22 Serikali itaimarisha utoaji wa mafunzo kwa vitendo na mazoezi ya kufundisha katika mafunzo ya ualimu.*

*5.2.23 Elimu ya ualimu itaimarishwa kwa kuwa na mamlaka itakayosimamia taaluma na maadili ya kazi ya ualimu.*

### Elimu ya Ufundi na Mafunzo

Elimu ya ufundi ni maarifa na stadi zinazohitajika katika ulimwengu wa kazi na ajira. Mafunzo ya ufundi yanajumuisha aina mbalimbali za stadi zinazohitajika katika jamii na soko la ajira.

#### Suala

Utoaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo.

#### Maelezo

Mafunzo ya ufundi hutolewa katika ngazi mbalimbali za utaalamu na kwa sekta tofauti. Programu na tuzo za mafunzo ya ufundi hazina muunganiko na mlinganisho madhubuti. Elimu na mafunzo ya ufundi hayajatolewa kwa kiwango cha kukidhi mahitaji katika sekta mbalmbali za uzalishaji na huduma. Kuna umuhimu wa kuimarisha utaoaji wa elimu hiyo katika ngazi za elimu-msingi ili kupata rasilimaliwatu stahiki kuendelea na mafunzo ya ufundi.

#### Madhumuni

Kuwa na elimu ya ufundi na mafunzo yenye muunganiko na inayokidhi mahitaji ya jamii.

Tamko

*5.2.24 Serikali itaimarisha utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo kwa kujumuisha stadi za ufundi katika ngazi zote za elimu.*

*5.2.25 Serikali itahakikisha kuwepo kwa muunganiko na mlinganisho wa programu za mafunzo ya ufundi katika mfumo wa elimu ya ufundi*

*5.2.26 Elimu ya Ufundi na Mafunzo itatolewa kwa kujumuisha Mafunzo ya fani na stadi mbalimbali kwa pamoja ili kuleta ufanisi katika utoaji wa elimu ya ufundi.*

*5.2.27 Utoaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo utaimarishwa kwa kuwa na programu za mafunzo kwa vitendo katika sekta za uzalishaji na za huduma.*

*5.2.28 Mfumo wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo utaimarishwa ili kuleta ulinganifu, muunganiko na ufanisi wa ngazi na fani mbalimbali za elimu ya ufundi*

Elimu ya Juu

Elimu ya Juu hutolewa baada ya elimu ya sekondari kwa lengo la kupata rasilimaliwatu yenye taaluma na utaalamu katika fani mbalimbali. Elimu hii hutolewa katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo na vyuo vikuu.

Suala

Utoaji fanisi wa Elimu ya Juu.

Maelezo

Sekta za uzalishaji na huduma zinahitaji wataalamu wenye elimu ya juu. Mahitaji ya wataalam katika sekta mbalimbali yanaongezeka mwaka hadi mwaka. Udahili katika mafunzo ya elimu ya juu hauna uwiano na ongezeko hili. Aidha, baadhi ya programu zinazotolewa hazizingatii mahitaji halisi ya vipaumbele vya jamii na taifa.

Katika karne hii utaalamu wa sayansi na teknolojia ndiyo msingi wa maendeleo katika nyanja zote. Pamoja na mwelekeo huo, hakuna maoteo halisi ya mahitaji ya

rasilimaliwatu kitaifa. Hali hii inafanya vyuo vya elimu ya juu kudahili wanafunzi bila mwongozo wa mahitaji ya kitaifa ya wataalamu wa aina mbalimbali na hivyo kusababisha kuwepo kwa baadhi ya progamu za mafunzo yasiyolenga mahitaji ya wataalamu.

Kuna umuhimu wa kuimarisha utoaji wa elimu ya juu kwa kuzingatia maoteo halisi ya kitaifa ya rasilimaliwatu kwa maendeleo ya nchi.

### Madhumuni

Kuwa na wataalamu wanaokidhi mahitaji ya jamii.

### Tamko

*5.2.29 Serikali itahakikisha kuwa rasilimali katika vyuo vya elimu ya juu zinatumika kwa ufanisi katika utoaji wa elimu ya juu.*

*5.2.30 Serikali itapanua nafasi za Elimu ya Juu kwa jinsi zote na makundi yenye mahitaji maalumu.*

*5.2.31 Serikali itahakikisha kuwa aina na ubora wa programu zinazotolewa katika elimu ya juu zinakidhi mahitaji ya jamii na taifa.*

*5.2.32 Serikali itaweka mazingira ya kuviwezesha vyuo vya Elimu ya Juu kutambuliwa kama vituo mahiri*

*5.2.33 Serikali itahakikisha kuwa utoaji wa elimu ya juu unazingatia maoteo halisi ya mahitaji ya wataalamu kitaifa.*

### Elimu ya Watu Wazima

Elimu ya Watu Wazima (EWW) hujumuisha utoaji wa maarifa na stadi za: kusoma, kuandika na kuhesabu; maisha, na kazi. Elimu ya watu wazima hutoa fursa kwa watu wazima kujiendeleza na kuendelea kujifunza katika muda wote wa maisha yao.

Suala

Utoaji wa elimu ya Watu Wazima kwa ufanisi.

Maelezo

Utoaji wa elimu ya watu wazima nchini unajumuisha elimu na shughuli za jamii kupitia Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya watu wazima na Jamii (MUKEJA). Mazingira ya kutolea elimu ya watu wazima kupitia MUKEJA yanaathiriwa na miundombinu isiyokidhi mahitaji ya watu wazima. Aidha, hakuna wataalamu stahiki wa kutosheleza mahitaji ya kutolea elimu hiyo.

Elimu ya kujiendeleza haijawafikia walengwa wote katika Jamii. Hali hii inasababishwa na upungufu wa miundombinu, rasilimaliwatu, fedha na vitendea kazi. Upo umuhimu wa kuimarisha utoaji wa elimu hii kwa wote.

Madhumuni

Kuwa na watu wazima wenye stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu (KKK) na wenye ari ya kujiendeleza.

*Tamko*

*5.2.34 Serikali itaimarisha utoaji wa Elimu ya Watu Wazima nchini.*

*5.2.35 Utoaji wa elimu ya watu wazima utazingatia mahitaji ya watu wazima katika jamii husika.*

## *5.3* Fursa na Usawa katika Utoaji wa Elimu na Mafunzo

Utoaji wa Elimu na mafunzo huzingatia fursa na usawa kwa rika na makundi yote. Hali kadhalika, hutilia mkazo ubora wa elimu na mafunzo yatolewayo ili kukidhi mahitaji ya jamii na kujenga utaifa. Ili kufanikisha uwepo wa fursa na usawa katika utoaji wa elimu na mafunzo, ni muhimu kuwa na shule na vyuo vyenye nyenzo na mazingira stahiki ili kukidhi uandikishaji na udahili wa makundi yote .

Suala

Fursa na usawa katika utoaji wa elimu na mafunzo

Maelezo

Utoaji wa elimu na mafunzo unazingatia upatikanaji wa nafasi za elimu na mafunzo bila ubaguzi wa jinsi, rangi, kabila, dini, hali ya kijamii au kipato ili kufikia malengo ya elimu na mafunzo kwa wote. Pamoja na juhudi za Serikali, sekta binafsi na washirika wa maendeleo kutoa nafasi za elimu kwa makundi yote, baadhi ya makundi bado hayajafikiwa kikamilifu kutokana na sababu za kijamii, kiuchumi na kijiografia. Hali hii inasababisha kutofikiwa kwa malengo ya kitaifa na kimataifa katika maendeleo.

Madhumuni

Kuwa na fursa na usawa katika utoaji wa elimu na mafunzo

Tamko

*5.3.1 Serikali itahakikisha upatikanaji wa elimu na mafunzo kwa usawa kwa makundi yote.*

*5.3.2 Serikali itaimarisha mazingira ya kushirikisha sekta binafsi na washirika wa maendeleo katika utoaji wa elimu na mafunzo.*

*5.3.3 Serikali itahakikisha kuwa wanafunzi wa jinsi zote wanatambuliwa, wanaandikishwa na wanahitimu elimu ya ngazi husika.*

Suala

Utaifa na uzalendo katika utoaji wa elimu na mafunzo.

Maelezo

Shule nyingi za msingi na sekondari ni za kutwa. Kwa hiyo, hazitoi nafasi ya kupokea wanafunzi kutoka kwenye maeneo mengine yaliyo mbali na shule hizo. Hali hiyo inapunguza uwezekano wa kuchanganyika kwa wanafunzi wenye utamaduni tofauti na hivyo kudhoofisha juhudi za kujenga na kuimarisha utaifa na uzalendo. Aidha, baadhi ya shule zisizo za Serikali zinaendeshwa kwa misingi ya ubaguzi na bila kuzingatia utaifa wa Tanzania.

Kwa hiyo kuna umuhimu wa kurekebisha hali hiyo ili kujenga na kuimarisha utaifa na uzalendo miongoni mwa wanafunzi na wananchi.

### Madhumuni

Kujenga na kuimarisha utaifa na uzalendo katika utoaji wa elimu.

### Tamko

*5.3.4 Serikali itahakikisha utoaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote unazingatia utaifa na uzalendo wa Mtanzania.*

### Suala

Utoaji wa Elimu na Mafunzo kwa makundi yenye mahitaji maalumu.

### Maelezo

Pamoja na jitihada za kutoa elimu kwa wote, baadhi ya makundi katika jamii yamekuwa hayapati elimu ipasavyo. Hali hii inatokana na mtindo wao wa maisha, hali ya uchumi na hali ya maumbile. Makundi hayo ni pamoja na wenye ulemavu, wanaoishi kwa mtindo wa kuhamahama na wanaoishi katika mazingira magumu. Kuna umuhimu wa kuondoa vikwazo vya kupata elimu na mafunzo kwa makundi hayo.

### Madhumuni

Kuondoa vikwazo vya kupata elimu na mafunzo kwa makundi yenye mahitaji maalumu.

### Tamko

*5.3.5 Serikali itaimarisha utoaji wa elimu na mafunzo kwa makundi yenye mahitaji maalumu.*

### Suala

Utoaji wa elimu na mafunzo kwa usawa wa kijinsia.

## Maelezo

Azma ya serikali ni kuwa na utoaji wa elimu na mafunzo unaozingatia usawa wa kijinsia katika ngazi zote za elimu na mafunzo. Kuna mdondoko wa wasichana na wavulana katika mfumo wa elimu kutokana na sababu mbalimbali, zikiwemo za ujauzito, ndoa za utotoni, ajira za watoto na utoro. Hata hivyo, ushiriki wa wasichana katika elimu unapungua kadiri wanavyoendelea katika ngazi za juu za elimu na mafunzo ukilinganishwa na ushiriki wa wavulana. Hali hii inahitaji marekebisho ili kufikia usawa wa kijinsia katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

## Madhumuni

Kuwa na usawa wa kijinsia katika utoaji wa elimu na mafunzo.

## Tamko

*5.3.6 Serikali itahakikisha kuwa utoaji wa elimu na mafunzo unazingatia usawa wa kijinsia.*

*5.3.7 Serikali itaondoa vikwazo vinavyozuia fursa ya wanafunzi kuendelea na masomo na kukamilisha mzunguko wa elimu katika ngazi husika.*

*5.3.8 Serikali itahakikisha kuwa wanafunzi wanaokatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo ujauzito na ugonjwa wanapata fursa ya kuendelea na elimu.*

*5.3.9 Serikali itahakikisha kuwa hatua stahiki zinachukuliwa dhidi ya watu watakaosababisha wanafunzi kukatisha masomo.*

*5.3.10 Serikali itahakikisha kuwa mitazamo na fikra mgando ya jinsia zinaondolewa katika mfumo wa elimu na mafunzo.*

## Elimu Jumuishi

Elimu jumuishi ni utaratibu wa utoaji wa elimu na mafunzo unaowafanya wanafunzi wote wawe sehemu ya jamii moja ya shule au chuo kwa kuzingatia mahitaji yao

bila ubaguzi. Tofauti zao hazipaswi kuwa kikwazo cha kupata elimu na mafunzo kwa usawa. Utaratibu huu unawafanya wanafunzi wa aina zote wajione kuwa wanakubalika na kila mmoja wao.

### Suala

Utoaji wa elimu jumuishi.

### Maelezo

Baadhi ya shule na vyuo vimewekewa miundombinu na vifaa na rasilimaliwatu stahiki ili kuwezesha kuwepo kwa elimu jumuishi. Hata hivyo, juhudi hizo hazijakidhi mahitaji ya utoaji wa elimu kwa makundi yenye mahitaji maalumu wakiwemo wenye ulemavu. Kutokana na ukosefu wa vifaa, miundombinu isiyokidhi mahitaji na upungufu wa rasilimaliwatu, utoaji wa elimu jumuishi nchini bado haujafikia kiwango stahiki. Aidha, upo utaratibu maalumu wa kuwahudumia wanafunzi wenye ulemavu wa aina tofauti wasioweza kuchanganyika na wengine ndani ya shule au chuo kwa mfano; wasioona, viziwi, wenye otizim na wenye ulemavu wa akili.

### Madhumuni

Kuimarisha utoaji wa elimu jumuishi nchini.

### Tamko

*5.3.11 Elimu jumuishi itakuwa ni sehemu ya mfumo wa elimu na mafunzo.*

*5.3.12 Serikali itaimarisha elimu jumuishi katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

### Elimu Nje ya Mfumo Rasmi

Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ni utaratibu wa utoaji wa elimu na mafunzo kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya kundi lengwa. Elimu hiyo hutolewa kwa utaratibu huria. Aidha, programu za elimu hii zina muundo wenye mpangilio maalumu na hutumia mbinu

shirikishi za kufundishia na kujifunzia.

Suala

Utoaji wa Elimu Nje ya Mfumo Rasmi.

Maelezo

Elimu Nje ya Mfumo rasmi hutolewa na taasisi na asasi za Serikali na zisizo za Serikali. Utoaji huo hufanyika kwa njia huria, masafa na ana kwa ana. Elimu hiyo hutolewa bila uratibu thabiti wa kitaifa hivyo kusababisha rasilimali isitumike kwa ufanisi na kuathiri viwango vya ubora wa elimu itolewayo.

Elimu itolewayo kwa utaratibu huria na kwa makundi fulani ya walengwa inahitaji uratibu thabiti ili iwe na muunganiko sahihi na ile itolewayo katika mfumo wa muda maalumu.

Madhumuni

Kuwa na uratibu thabiti wa utoaji wa Elimu na mafunzo nje ya Mfumo rasmi.

Tamko

*5.3.13 Elimu kwa njia huria, masafa na ana kwa ana itakuwa ni sehemu ya mfumo wa elimu na mafunzo*

*5.3.14 Serikali itaimarisha utoaji wa elimu kwa njia huria na kwa masafa kwa ngazi zote za elimu na mafunzo.*

## *5.4* Mitaala ya Elimu na Mafunzo

Mtaala wa elimu ni jumla ya mambo ambayo mlengwa anatakiwa kuyapata katika mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa lengo la kufikia matarajio ya jamii na taifa. Utekelezaji wa mitaala ya elimu na mafunzo hutumia mihtasari. Muhtasari ni mpangilio wa malengo, maudhui, mchakato na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa kila somo na ngazi ya elimu na mafunzo.

Suala

Mitaala stahiki ya elimu na mafunzo

Maelezo

Mitaala ya elimu na mafunzo inatarajiwa kumpa mwanafunzi maarifa, stadi na mwelekeo stahiki. Mitaala haina budi kuzingatia maeneo ya utafiti, sayansi na teknolojia, stadi za teknolojia asili, TEHAMA na michezo. Vile vile, mitaala iliyopo haitoshelezi kumpa mlengwa maarifa, stadi na mwelekeo na kumwezesha kukabiliana kikamilifu na changamoto za maendeleo. Aidha, baadhi ya programu katika vyuo hazina muunganiko na mlinganisho wa kimaudhui katika baadhi ya ngazi za elimu na mafunzo.

Katika vituo vya kulelea watoto wadogo elimu inayotolewa haina uratibu madhubuti wa kuiwezesha kuweka misingi sahihi ya elimu na mafunzo. Kuna umuhimu wa kuimarisha maudhui, mchakato, vifaa vya kufundishia na kujifunzia ili kuleta tija na ufanisi katika utoaji wa elimu.

Madhumuni

Kuwa na mitaala inayokidhi mahitaji katika mfumo wa elimu na mafunzo.

Tamko.

*5.4.1 Serikali itaimarisha ukuzaji, utayarishaji na utekelezaji wa mitaala kwa kuzingatia mahitaji ya taifa na ya walengwa katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

*5.4.2 Uandaaji na utekelezaji wa mitaala utazingatia umahiri wa kumudu stadi katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

*5.4.3 Serikali itahakikisha kuwa mtaala wa Elimu katika vituo vya kulelea watoto wadogo unaandaliwa ili kukidhi mahitaji ya watoto na jamii*

*5.4.4 Elimu na mafunzo ya maadili, uzalendo na utaifa itakuwa ni sehemu ya mitaala katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

*5.4.5 Stadi za ujasiriamali zitakuwa ni sehemu ya programu zote za Elimu na Mafunzo.*

*5.4.6 Serikali itaimarisha udhibiti wa ubora na ulinganifu wa mitaala ya asasi za elimu ya juu ili kuleta ufanisi wa programu*

*zitolewazo.*

*5.4.7 Serikali itahakikisha kuwa mitaala ya elimu ya watu wazima na ya kujiendeleza inakidhi mahitaji ya kundi hilo.*

*5.4.8 Serikali itahakikisha kuwa michezo inaendelea kuwa sehemu ya mitaala katika shule na vyuo.*

### Elimu ya Sayansi na Teknolojia

#### Suala

Utoaji wa elimu ya sayansi na teknolojia

#### Maelezo

Sayansi na teknolojia ni nyenzo muhimu katika kumwezesha binadamu kumudu mazingira yake na kumwezesha kuwa na maendeleo. Shule na vyuo vina majukumu muhimu ya kukuza elimu ya sayansi na teknolojia. Mitaala ya shule na vyuo inaweka mkazo katika ufundishaji wa hisabati, sayansi yakiwemo masomo ya fizikia, kemia, biolojia, TEHAMA. Katika vyuo vikuu, ufundishaji wa programu za sayansi na teknolojia unategemea aina na uwezo wa chuo husika.

Ufundishaji wa masomo katika shule na programu katika vyuo unakabiliwa na uhaba wa rasilimaliwatu, vifaa na miundombinu stahiki. Aidha, hakuna uwiano kati ya programu zinazotolewa na mahitaji halisi ya soko la ajira kutokana na kutokuwepo kwa utaratibu wa kitaifa wa kubaini na kupanga maoteo ya rasilimaliwatu ikiwa ni pamoja na taaluma ya sayansi na teknolojia.

#### Madhumuni

Kuwa na jamii yenye elimu ya Sayansi na teknolojia.

#### Tamko

*5.4.9 Ufundishaji wa hisabati, sayansi na teknolojia utaimarishwa katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

*5.4.10 Masomo ya sayansi, hisabati na teknolojia yatakuwa sehemu ya mitaala ya elimu na mafunzo katika ngazi zote za elimu na*

*mafunzo.*

*5.4.11 Stadi za utafiti zitakuwa sehemu ya mitaala ya shule, vyuo na taasisi za elimu na Mafunzo.*

Sayansi Jamii

Suala

Utoaji wa elimu ya sayansi jamii.

Maelezo

Sayansi jamii humwezesha mtu kujitambua, kutambua wajibu na haki zake, kuelewa mabadiliko ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kiteknolojia. Sayansi jamii hufundishwa katika ngazi zote za elimu na mafunzo kwa njia ya masomo tofauti. Aidha, kuna upungufu wa ufundishaji wa sayansi jamii unaochagizwa na upungufu wa rasilimaliwatu, vitendea kazi na miundombinu stahiki. Kuna umuhimu wa kuimarisha utoaji wa elimu ya sayansi jamii ili ukidhi mahitaji ya wanafunzi na soko la ajira.

Madhumuni

Kuwa na jamii yenye elimu ya sayansi-jamii inayokidhi mahitaji ya taaluma na utaalamu katika soko la ajira.

Tamko

*5.4.12 Elimu ya sayansi-jamii itakuwa ni ya lazima katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

*5.4.13 Serikali itahakikisha kuwepo kwa uwiano stahiki katika masomo ya sayansi na sayansi jamii katika mfumo wa elimu na mafunzo*

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

Suala

TEHAMA katika elimu na mafunzo

Maelezo

TEHAMA ni teknolojia ya habari na mawasiliano inayowezesha kuhifadhi, kubadilishana habari, kufundisha na kujifunzia, na kurushia matangazo kwa njia ya mtandao kwa kutumia mitambo ya teknolojia ya kisasa kama vile redio, televisheni, satelaiti, video, simu na kompyuta.

Mahitaji ya TEHAMA katika ngazi zote za elimu yameongezeka kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia pamoja na utandawazi. Hata hivyo, miundombinu na rasilimali zilizopo nchini na kwenye taasisi za elimu na mafunzo haikidhi mahitaji ya ongezeko la watumiaji na mabadiliko ya haraka ya teknolojia.

Madhumuni

Kuwa na TEHAMA katika elimu na mafunzo.

Tamko

*5.4.14* TEHAMA itaendelea kuwa sehemu ya mitaala ya elimu na mafunzo katika ngazi zote.

*5.4.15* *Serikali itaimarisha matumizi ya TEHAMA katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

Nyenzo za kufundishia na kujifunzia

Nyenzo za kujifunzia na kufundishia ni vitabu na vifaa mbalimbali vinavyotumika katika kutekeleza mitaala ya elimu na mafunzo.

Suala

Ubora wa nyenzo za kufundishia na kujifunzia

Maelezo

Utekelezaji wa mitaala unategemea upatikanaji wa vitabu na nyenzo nyingine stahiki za kufundishia na kujifunzia. Katika dunia ya utandawazi kuna vyanzo mbalibmali vya kupatia maarifa ikiwa ni pamoja na vitabu vya kawaida na vya kielekroniki na mitandao mbalimbali. Aidha, baadhi ya vifaa vilivyoko sokoni havina ubora stahiki kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia makundi yote katika shule na

vyuo vya ualimu. Katika hali hii upo umuhimu wa kuchuja na kudhibiti ubora wa vifaa na maandiko yanayoingia katika mfumo wa kufundisha na kujifunza.

### Madhumuni

Kuwa na vitabu na nyenzo nyingine zinazokidhi mahitaji

### Tamko

*5.4.16 Serikali itadhibiti ubora wa vitabu na nyenzo nyingine za kufundishia na kujifunzia.*

*5.4.17 Serikali itahakikisha upatikanaji fanisi wa vitabu na nyenzo nyingine stahiki za kufundishia na kujifunzia katika elimu na mafunzo.*

*5.4.18 Serikali itaimarisha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa watu wenye ulemavu na wenye mahitaji mengine maalumu.*

### Huduma za Maktaba

Huduma za maktaba ni moja ya nyenzo ya kufundishia na kujifunzia ambayo humwezesha mtu kupata maarifa, stadi na mwelekeo

### Suala

Utoaji wa huduma stahiki za Maktaba.

### Maelezo

Huduma za maktaba hutoa fursa ya kukuza tabia na mwenendo wa usomaji na kujifunza, kuimarisha ufundishaji, kuongeza maarifa na kujiendeleza. Huduma bora za maktaba zinatambulika kwa kuwepo kwa miundombinu stahiki, vitabu na machapisho mengine na rasilimali stahiki na za kutosha kwa matumizi ya uendeshaji.

Kuongezeka kwa fursa za elimu pamoja na kasi ya kukua kwa sayansi na teknolojia kumeongeza mahitaji ya matumizi ya maktaba. Hata hivyo, huduma za maktaba hazijaweza kukidhi mahitaji ya umma katika ngazi zote za shule na jamii.

Madhumuni

Kuwa na huduma bora za maktaba katika shule, vyuo na maeneo mengine katika jamii.

Tamko

*5.4.19 Serikali itaimarisha utoaji wa huduma za maktaba kwa shule na jamii.*

*5.4.20 Serikali itaanzisha na kuendeleza huduma za maktaba za umma zitakazokidhi mahitaji ya makundi yote ya jamii.*

## *5.5* Lugha katika Elimu na Mafunzo

Matumizi ya lugha katika elimu na mafunzo.

Lugha ni chombo cha mawasiliano na nyenzo muhimu ya kupata mbinu-tambuzi, maarifa, teknolojia, mitazamo na maadili. Kiingereza na Kiswahili ni lugha zinazotumika kwa kufundishia na kujifunzia katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo.

Suala

Ufundishaji wa lugha.

Maelezo

Lugha za kiswahili, Kiingereza na lugha nyingine za kigeni zinafundishwa kama masomo katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo. Pamoja na juhudi za kufundisha lugha hizo, bado kuna udhaifu wa kumudu lugha sanifu katika mawasiliano. Sehemu kubwa ya udhaifu huo inatokana na mbinu duni za kufundishia, umahiri mdogo na matumizi madogo ya lugha sanifu katika mazingira ya kawaida.

Lugha ya Kiswahili inatumika kama lugha ya kwanza au ya pili miongoni mwa wananchi wengi. Aidha, Kiswahili ni lugha ya taifa. Lugha ya Kiswahili imekua kwa kiwango cha kimataifa ambapo inaweza kutumiwa na wananchi wengi kupata maarifa katika nyanja mbalimbali, ikiwa ni pamoja na sayansi na teknolojia. Lugha ya Kiingereza inatumika kama lugha ya pili kwa baadhi ya wananchi. Kiswahili na

Kiingereza ni lugha rasmi za kiofisi. Kiswahili, Kiingereza na lugha nyingine za kigeni zitawezesha watanzania kuwa na mawasiliano na watu wa mataifa mengine na kupata maarifa. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuimarisha ufundishaji wa lugha za Kiswahili, Kiingereza na lugha nyingine za kigeni.

### Madhumuni

Kuimarisha ufundishaji wa lugha kwa ajili ya kuwasiliana, kufundishia na kujifunzia.

### Tamko

*5.5.1 Serikali itaimarisha ufundishaji wa lugha za Kiswahili, Kiingereza na lugha nyingine za kigeni katika mfumo wa elimu na mafunzo.*

### Suala

Lugha ya kufundishia

### Maelezo

Lugha za kufundishia na kujifunzia katika elimu na mafunzo ni Kiswahili na Kiingereza. Lugha ya kufundishia elimu ya awali na msingi ni Kiswahili. Aidha, lugha ya Kiingereza inatumika kufundishia katika baadhi ya shule.

Lugha ya Kiingereza hutumika kufundishia katika shule za sekondari, vyuo vya ualimu ngazi ya stashahada, vyuo vya ufundi na vyuo vya elimu ya juu. Aidha, lugha ya Kiswahili hutumika kufundishia katika vyuo vya mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti na vyuo vya ufundi stadi.

Matumizi ya lugha ya Kiingereza yanazidi kupanuka ulimwenguni kutokana na utandawazi. Hali kadhalika, matumizi ya Kiswahili nchini na katika mabara mengine yameongezeka. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuimarisha matumizi ya lugha za Kiswahili na Kiingereza kwa kuzifanya kuwa lugha za kufundishia katika ngazi mbalimbali.

Madhumuni

Kuimarisha ufundishaji kwa kutumia lugha stahiki

Tamko

*5.5.2 Lugha ya kufundishia elimu ya awali itakuwa Kiswahili.*

*5.5.3 Lugha za kufundishia Elimu ya Msingi zitakuwa Kiswahili na Kiingereza.*

*5.5.4 Lugha za kufundishia kwa ngazi ya Elimu ya Sekondari itakuwa Kiswahili na Kiingereza.*

*5.5.5 Lugha za kufundishia elimu ya ualimu zitakuwa ni Kiswahili na Kiingereza.*

*5.5.6 Programu ya Stadi za Mawasiliano itakuwa ni ya lazima kwa elimu ya ualimu.*

*5.5.7 Serikali itaimarisha mafunzo ya lugha za Kiswahili, Kiingereza na lugha nyingine za kigeni kwa walimu.*

*5.5.8 Lugha ya kufundishia elimu ya ufundi na mafunzo itaendelea kuwa Kiingereza na Kiswahili.*

*5.5.9 Lugha ya kufundishia elimu ya juu itakuwa Kiingereza .*

Lugha ya alama

Suala

Matumizi ya lugha ya alama

Maelezo

Lugha ya alama hutumika kufanya mawasiliano baina ya viziwi na watu wengine. Wanafunzi viziwi wanashindwa kupata elimu na mafunzo kwa ufanisi kutokana na kutokuwepo na utaratibu mahsusi wa kufundisha na kutumia lugha ya alama katika elimu na mafunzo.

Madhumuni

Uimarishaji wa lugha ya alama katika elimu na mafunzo

Tamko

*5.5.10 Lugha ya alama itakuwa lugha rasmi katika mfumo wa elimu na mafunzo.*

*5.5.11 Serikali itaimarisha matumizi ya lugha ya alama katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

## *5.6* Upimaji, Tathmini na Utoaji Vyeti

Upimaji katika elimu na mafunzo hutumia njia mbalimbali zikiwemo mitihani, mazoezi, majaribio na utafiti. Matokeo ya upimaji huwezesha kutathmini utendaji wa mwanafunzi, mwalimu, shule au chuo katika utekelezaji wa mitaala. Aidha, matokeo ya tathmini hutumika katika maamuzi ya kupanga, kuchagua na kutunuku vyeti.

Suala

Upimaji na tathmini ya Elimu na Mafunzo.

Maelezo

Upimaji na tathmini katika elimu na mafunzo unatumia njia mbalimbali ambazo hutofautiana kulingana na ngazi, fani na aina ya kozi. Uhalali wa matokeo ya upimaji na tathmini unategemea uthabiti na ukamilifu wa kila hatua ya mchakato wa upimaji. Upimaji na tathmini hufanywa na shule na vyuo na kuratibiwa na taasisi zilizopewa dhamana hiyo.

Aidha, Vyuo Vikuu na taasisi za elimu ya ufundi na mafunzo zina mamlaka ya upimaji, tathmini na utoaji tuzo baada ya programu zao kupewa ithibati na mamlaka husika. Hali hii inaweza kutoa mwanya wa kutokuwepo kwa ulinganifu katika viwango vya upimaji na tathmini baina ya vyuo; programu na tuzo

zinazofanana. Aidha, upimaji na tathmini unatakiwa kuzingatia ustadi na umahiri wa mwanafunzi katika ngazi husika.

Kutokana na umuhimu wa upimaji na tathmini katika elimu na mafunzo, hakuna budi kuwa na utaratibu wa kitaifa wa kudhibiti upimaji na tathmini katika ngazi na programu mbalimbali za elimu na mafunzo.

### Madhumuni

Kuwa na udhibiti na uratibu thabiti wa upimaji na tathmni ya elimu na mafunzo

### Tamko

*5.6.1 Serikali itaimarisha upimaji na utoaji vyeti kwa elimu-msingi.*

*5.6.2 Serikali itaimarisha upimaji na tathmini ya EWW nchini.*

*5.6.3 Upimaji na tathmini ya elimu ya ualimu, ufundi na elimu ya juu utazingatia maarifa na ustadi katika ngazi husika.*

*5.6.4 Serikali itaweka na kusimamia mfumo wa kitaifa wa sifa linganifu wa tuzo na vyeti kwa ngazi zote za Elimu na Mafunzo*

*5.6.5 Msingi wa kupata cheti cha kuhitimu ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo utakuwa ni upimaji na tathmini ya kila siku na matokeo ya mwisho ya upimaji huo.*

## Mitihani na Tuzo za Nje

### Suala

Uratibu na udhibiti wa mitihani na tuzo za nje.

### Maelezo

Mitihani ya bodi mbalimbali za mitihani ya nje katika ngazi za taaluma na utaalamu huratibiwa na Baraza la Mitihani Tanzania. Aidha, baadhi ya shule na vyuo visivyo vya serikali hutumia mitihani ya nje kwa baadhi ya wanafunzi wake. Kutokana na

kupanuka kwa teknolojia, baadhi ya watu wamekuwa wakifanya mitihani ya nje kupitia mtandao. Vile vile, kuna shule, vyuo na vituo ambavyo vinaendesha mitihani ya nje bila kutambuliwa rasmi. Hali hii inafanya udhibiti wa uendeshaji wa mitihani hiyo ya nje na viwango vya elimu na mafunzo wanavyofikia wanafunzi hao kuwa mgumu. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kudhibiti tuzo; na mitihani ya nje inayofanyika nchini.

Madhumuni

Kuwa na uratibu na udhibiti madhubuti wa Mitihani na Tuzo za Nje.

Tamko

*5.6.6 Serikali itaimarisha uratibu wa mitihani na udhibiti wa tuzo na vyeti vya nje katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

## *5.7* Uongozi na Utawala wa Elimu na Mafunzo.

### Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu na Mafunzo

Usimamizi na uendeshaji wa elimu na mafunzo nchini ni jukumu la Wizara yenye dhamana ya Elimu na Mafunzo. Usimamizi na uendeshaji wa shule, vyuo na taasisi nyingine za elimu na mafunzo hufanywa kwa kushirikiana na wizara nyingine, mashirika na taasisi za Serikali na zisizo za Serikali. Aidha, usimamizi na uendeshaji wa shule za msingi na sekondari za Serikali unafanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Taasisi na mashirika yaliyopo chini ya wizara yenye dhamana ya elimu na mafunzo yana mamlaka kamili ya kuendesha shughuli zake bila uhusiano wa kisheria baina yao. Hali kadhalika, mashirika na taasisi zisizo za serikali ambazo hutoa na kuendesha elimu na mafunzo husajiliwa na kutambuliwa rasmi na vyombo vya Serikali vilivyopewa dhamana hiyo. Kutokana na mahusiano yaliyopo na ukubwa wa sekta ya elimu na mafunzo, kuna umuhimu wa kuimarisha uratibu kwa kufungamanisha ngazi zote za elimu na sekta anuwai.

### Suala

Udhibiti wa ubora wa elimu na mafunzo .

### Maelezo

Wizara yenye dhamana ya elimu na mafunzo ina taasisi na mashirika yanayosimamia na kuratibu utoaji wa elimu na mafunzo. Kila taasisi na mashirika hayo yana bodi za utendaji ambazo hutoa maamuzi juu ya masuala ya utoaji na uendeshaji wa elimu na mafunzo katika maeneo ya mamlaka zao.Taasisi hizo zina majukumu ya utambuzi rasmi wa vyuo, uandaaji wa mitaala, utoaji wa mitihani, tuzo na vyeti kwa pamoja katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo. Aidha, zipo taasisi ambazo husimamia ubora wa elimu na mafunzo na wakati huo huo humiliki vyuo vinavyotoa elimu na mafunzo hayo. Matokeo yake ni mwingiliano wa majukumu unaoathiri uwajibikaji na ubora wa elimu na mafunzo yatolewayo. Hali hii inaathiri ubora wa elimu na mafunzo yatolewayo, na hivyo, husababisha kutokutambulika kwa baadhi ya tuzo zitolewazo na kuleta ugumu wa kukubalika kwa wahitimu kuendelea na elimu na mafunzo katika ngazi zinazofuata.

### Madhumuni

Kuwa na ufanisi katika usimamizi wa utoaji wa elimu na mafunzo.

### Tamko

*5.7.1 Utambuzi rasmi wa shule na vyuo; uandaaji wa mitaala; upimaji; utoaji tuzo na vyeti utasimamiwa na mamlaka ya kitaifa itakayokasimiwa madaraka hayo.*

### Ukaguzi wa Shule

Ukaguzi wa shule na vyuo ni uhakiki wa viwango na mwenendo wa utoaji wa elimu na mafunzo kwa kuzingatia mitaala iliyopo na taratibu za uendeshaji. Wizara yenye dhamana ya elimu na mafunzo hutumia mamlaka mbalimbali kukagua shule na vyuo kwa lengo la kutumia taarifa za ukaguzi kudhibiti ubora wa elimu. Hivyo

ukaguzi ni muhimu katika kuhakikisha utoaji wa elimu na mafunzo bora.

Suala

Ukaguzi wa viwango vya utoaji wa elimu na mafunzo.

Maelezo

Udhibiti wa ubora wa elimu na mafunzo katika shule na vyuo vya ualimu unafanywa na Wizara kwa kupitia idara ya Ukaguzi wa shule. Udhibiti huu hauna uthabiti na ufanisi unaostahili kutokana na idara hiyo kuwa sehemu ya Wizara inayokaguliwa utendaji wake. Aidha, Tume ya Vyuo Vikuu na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi vimepewa majukumu ya utambuzi rasmi wa vyuo na kuthibitisha programu mbalimbali katika vyuo hivyo. Wizara pamoja na taasisi nyingine za elimu na mafunzo zinatumia vyombo vya ndani kujikagua. Utaratibu huu wa wizara na taasisi kujiwekea viwango, kutekeleza na kuhakiki ubora wa utekelezaji wake unadhoofisha uwezo wa kuibua upungufu katika utoaji wa elimu na mafunzo.

Madhumuni

Kuimarisha udhibiti wa ubora wa elimu na mafunzo.

Tamko

*5.7.2 Ukaguzi wa shule na vyuo katika ngazi zote za Elimu na Mafunzo utafanywa na kusimamiwa na mamlaka itakayokasimiwa madaraka hayo.*

*5.7.3 Serikali itaimarisha ukaguzi wa shule kwa lengo la kudhibiti ubora wa elimu itolewayo*

Suala

Mazingira na huduma muhimu shuleni na vyuoni.

Maelezo

Utoaji wa elimu na mafunzo unahitaji mazingira yenye utulivu na usalama. Shule na vyuo vinapaswa kuwa kwenye mazingira stahiki na yenye huduma muhimu ili

kuwezesha utoaji wa elimu kwa ufanisi . Mazingira katika baadhi ya shule na vyuo nchini ni duni na hayana usalama wa kutosha. Aidha, kuna upungufu mkubwa wa huduma muhimu kama chakula, maji safi na salama, afya, umeme, mawasiliano na usafiri. Huduma hizi huongeza ushiriki katika elimu na mafunzo. Kuna umuhimu wa kuwa na mazingira yanayokidhi mahitaji na huduma muhimu shuleni na vyuoni ili kuinua ubora wa elimu na mafunzo.

### Madhumuni

Kuwa na mazingira salama na huduma muhimu na endelevu shuleni na vyuoni.

### Tamko

*5.7.4 Serikali itahakikisha kuwa huduma muhimu zikiwemo za chakula bora, mawasiliano, umeme, maji safi na salama, na afya zinapatikana katika shule na vyuo.*

*5.7.5 Mazingira bora na yenye usalama yatakuwa ni ya lazima katika utoaji wa elimu na mafunzo.*

## Baraza la Ushauri la Elimu na Mafunzo

### Suala

Utaratibu wa kuishauri Wizara.

### Maelezo

Serikali inahitaji kushauriwa kwa upeo mpana katika masuala yanayohusu elimu na mafunzo. Ushauri huo unaweza kupatikana kwa kuwa na chombo ambacho kitajumuisha wadau wenye upeo na uzoefu wa elimu na mafunzo kutoka sekta za Serikali na zisizo za Serikali. Baraza la Ushauri la Elimu linateuliwa na waziri mwenye dhamana ya elimu na wajumbe wake wanateuliwa na waziri kadiri atakavyoona inafaa (Sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978). Utaratibu huu unaruhusu udhaifu katika uteuzi wa wajumbe wa baraza. Baraza lililopo halina sekretarieti. Hali hii inasababisha baraza lishindwe kutoa ushauri ipasavyo.

Madhumuni

Kuwa na chombo madhubuti cha ushauri wa elimu.

Tamko

*5.7.6 Serikali itaimarisha Baraza la Ushauri wa Elimu na Mafunzo litakaloibua hoja na kushauri ipasavyo kuhusu usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini.*

*5.7.7 Kutakuwa na sekretariati imara ya Baraza la ushauri wa elimu na mafunzo itakayoratibu shughuli za Baraza hilo.*

*Suala*

Usimamizi na uendeshaji madhubuti wa shule na vyuo

Maelezo

Usimamizi na uendeshaji wa asasi za elimu na mafunzo, kwa sehemu kubwa, umekuwa ukifanywa na viongozi wa asasi husika; na ushirikishaji wa jamii hutegemea utashi wa uongozi wa shule au chuo. Ni muhimu kurekebisha hali hii kwa kuimarisha kamati na bodi  za asasi hizo, ili wakuu wa asasi wawajibike kwa vyombo hivyo. Aidha, wazazi ni wadau wakuu katika utoaji wa elimu na malezi ya wanafunzi. Aghalabu, uhusiano mzuri kati ya mwalimu na mzazi huimarisha maendeleo ya mwanafunzi.

Madhumuni

Kuwa na shule na vyuo vinavyoendeshwa kwa ufanisi .

Tamko

*5.7.8 Shule za msingi zitaendelea kuwa na Kamati; na shule za sekondari na vyuo vya ualimu na ufundi vitaendelea kuwa na Bodi zitakazosimamia uendeshaji wake.*

*5.7.9 Kutakuwa na Vyama vya mahusiano mema kati ya wazazi/walezi na walimu katika shule za msingi na sekondari.*

Suala

Viongozi wa elimu na mafunzo.

Maelezo

Uongozi na utawala bora ni muhimu kwa ufanisi wa mfumo wa elimu na mafunzo. Viongozi wa elimu na mafunzo kwenye ngazi za taifa, mkoa, wilaya na asasi sharti wawe na uzoefu, maadili na sifa za kitaaluma, kitaalamu na ujuzi katika uongozi na utawala wa elimu na mafunzo. Kuna umuhimu wa kuwa na viongozi wenye sifa stahiki ili kuleta ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa elimu na mafunzo.

Madhumuni

Kuwa na viongozi wenye sifa stahiki.

Tamko

*5.7.10 Nafasi za uongozi wa elimu ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na shule zitapewa madaraka ya utekelezaji wa sera ya elimu na mafunzo.*

*5.7.11 Viongozi wa elimu na mafunzo katika ngazi mbalimbali watapaswa kuwa na sifa stahiki za kitaaluma, kitaalamu na uongozi.*

Suala

Hadhi maalumu katika utumishi kwa viongozi katika ngazi mbalimbali za Elimu na Mafunzo.

Maelezo

Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo husimamiwa katika ngazi mbalimbali. Baadhi ya nafasi za uongozi katika ngazi hizo, mathalani; mkoa, shule za msingi na sekondari hazitambuliwi rasmi katika utumishi wa umma. Hali hii inapunguza hadhi na ari ya utendaji katika nafasi hizo. Kuna umuhimu wa kuinua hadhi ya nafasi zao ili kuimarisha usimamizi na utendaji wa kazi.

Madhumuni

Kuwa na wasimamizi wa utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo wenye hadhi maalumu katika utumishi.

Tamko

*5.7.12 Nafasi za usimamizi wa utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo katika ngazi mbalimbali zitakuwa na hadhi maalumu katika utumishi.*

Suala

Utumishi wa walimu na wakufunzi.

Maelezo

Utumishi wa walimu na wakufunzi unasimamiwa na mamlaka ya ajira na mwajiri. Mamlaka ya utumishi wa walimu ni Tume ya Utumishi wa Umma - Idara ya Utumishi wa Walimu. Waajiri wa walimu ni pamoja na Serikali Kuu, Halmashauri, Mashirika na Taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Serikali. Mamlaka hizo zina mawasiliano hafifu kuhusu stahili za mwalimu ikiwa ni pamoja na kupandishwa ngazi ya utumishi, nyongeza ya mshahara na maslahi mbalimbali. Hali hii inasababisha walimu kuchelewa kupata stahili zao na wakati mwingine kuzikosa kabisa.

Madhumuni

Kuwa na ufanisi katika utumishi wa walimu.

Tamko

*5.7.13 Mwajiri wa walimu atahusika na taratibu zote za kiutumishi za mwalimu.*

*5.7.14 Utambuzi rasmi wa walimu wenye vyeti wa shule na vyuo vya Serikali na visivyo vya Serikali utafanywa na mamlaka iltakayokasimiwa madaraka hayo.*

Suala

Menejimenti ya data za Elimu na Mafunzo.

Maelezo

Menejimenti ya data inahusisha uratibu wa ukusanyaji, uchambuzi, uhifadhi na usambazaji wa data na taarifa. Hifadhi-data inawezesha uwepo wa data unganifu kutoka taasisi na asasi za elimu na mafunzo. Uwepo wa mfumo madhubuti wa menejimenti ya data unachangia kwa kiasi kikubwa kuleta ufanisi katika uendeshaji wa elimu na mafunzo. Kuna vyanzo vingi vya data za kielimu ambavyo data zake hazina uhakiki na uratibu madhubuti. Hali hii inapunguza usahihi, uhakika na ufananivu wa data kwa wakati. Ni muhimu data na taarifa mbalimbali za Elimu na Mafunzo kukusanywa, kuchambuliwa na kuhifadhiwa vizuri ili ziweze kupatikana na kutumiwa na wadau mbalimbali kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Madhumuni

Kuwa na mfumo madhubuti wa menejimenti ya data za Elimu na Mafunzo.

Tamko

*5.7.15 Serikali itaweka mfumo madhubuti wa menejimenti ya data za elimu na mafunzo.*

Suala

Ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

### Maelezo

Elimu ya Juu ni suala la muungano, wakati ngazi nyingine za elimu sio za muungano. Hata hivyo sekta za Elimu Tanzania Bara na Tanzania Visiwani zina uhusiano na ushirikiano katika maeneo ya mitaala na upimaji wa elimu ya ufundi na mafunzo. Hali kadhalika, katika ngazi ya elimu ya sekondari na vyuo vya ualimu kuna uhusiano katika maeneo ya mitaala, upimaji na utoaji vyeti. Kwa kuzingatia hali hiyo, kuna umuhimu wa kuimarisha uhusiano na ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

### Madhumuni

Kuimarisha ushirikiano na uhusiano wa kielimu kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

### Tamko

*5.7.16 Ushirikiano katika Elimu na Mafunzo kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar utaimarishwa.*

## Ardhi kwa Matumizi ya Kielimu

### Suala

Hatimiliki za ardhi kwa asasi za elimu na mafunzo.

### Maelezo

Asasi za elimu na mafunzo zinahitaji kumilikishwa ardhi ya kutosha kwa mahitaji ya sasa na maendeleo ya baadaye. Ardhi inayomilikishwa inatakiwa kuwa katika mazingira ya amani, utulivu na usalama ili kuhakikisha utoaji wa elimu bora. Asasi nyingi za elimu na mafunzo ziko kwenye ardhi ambayo haijamilikishwa kwao. Aidha, kumekuwepo na tabia ya uvamizi wa ardhi iliyotengwa kwa ajili ya asasi za elimu na mafunzo za Serikali na zisizo za Serikali. Ili kulinda ardhi za taasisi za elimu na mafunzo zisivamiwe, kuna umuhimu kwa asasi zote za elimu na mafunzo kuwa na

umiliki wa ardhi kisheria.

Madhumuni

Kuwa na asasi za elimu na mafunzo zenye hatimiliki za ardhi.

Tamko

*5.7.17 Kila Asasi ya elimu na mafunzo itatakiwa kuwa na hatimiliki ya ardhi ilipo asasi hiyo.*

*5.7.18 Serikali itaimarisha upatikanaji wa hatimiliki ya ardhi kwa ajili ya asasi za elimu na mafunzo.*

## *5.8* Uwezo katika Utoaji wa Elimu na mafunzo

Uwezo wa utendaji katika elimu na mafunzo unajumuisha rasilimaliwatu, fedha, miundombinu na vitendea kazi. Baadhi ya viongozi wa elimu katika ngazi mbalimbali hawana sifa na ujuzi wa kutosha ili kutekeleza majukumu ya usimamizi na uendeshaji wa elimu na mafunzo. Aidha, kuna upungufu mkubwa wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, na miundombinu isiyokidhi mahitaji. Hali hii inaathiri uwezo wa utoaji wa elimu bora

Suala

Upatikanaji wa rasilimaliwatu.

Maelezo

Kupanuka kwa sekta rasmi na isiyo rasmi kumeongeza shughuli nyingi za kiuchumi ambazo zinahitaji rasilimaliwatu yenye maarifa, stadi na ujasiriamali. Kutokana na mabadiliko katika sayansi na teknolojia na kuongezeka kwa mahitaji ya watendaji wenye sifa mbalimbali, utoaji wa elimu na mafunzo hauna budi kukidhi mahitaji hayo.

Uwezo wa utoaji wa elimu na mafunzo unaathiriwa na upungufu wa rasilimaliwatu

yenye sifa zinazokidhi mahitaji. Hali hii inasababishwa na uwezo mdogo wa taasisi kuandaa rasilimaliwatu na baadhi ya wataalam wa elimu na mafunzo kuacha kazi kutokana na mazingira ya ajira na kazi yasiyovutia.

### Madhumuni

Kuwa na rasilimaliwatu yenye kukidhi mahitaji.

### Tamko

*5.8.1 Serikali itahakikisha kuwepo kwa rasilimaliwatu yenye sifa stahiki katika ngazi zote za Elimu na Mafunzo.*

*5.8.2 Mafunzo kabilishi na rejeshi kwa watumishi wa ngazi zote za Elimu na Mafunzo yatakuwa ya lazima.*

*5.8.3 Serikali itaimarisha utoaji wa mafunzo ya menejimenti ya elimu na mafunzo kwa viongozi wa ngazi zote.*

*5.8.4 Serikali itaimarisha mazingira ya kazi na ajira, na maslahi ya rasilimaliwatu katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

### Suala

Miundombinu katika elimu na mafunzo.

### Maelezo

Uwepo wa miundombinu ya kutosha na yenye viwango vya ubora stahiki ni muhimu katika kuinua ubora wa Elimu na Mafunzo katika ngazi zote. Miundombinu iliyopo katika shule, vyuo na taasisi nyingi za elimu na mafunzo ikiwemo majengo, mifumo ya maji, umeme na barabara imechakaa na haitoshelezi mahitaji ya makundi yote. Mipango ya maendeleo ya elimu na mafunzo iliyopo haitoshelezi mahitaji ya miundombinu kulingana na ongezeko la watumiaji. Aidha, jamii haina utamaduni wa utunzaji na uhifadhi na matengenezo ya mara kwa mara ya miundombinu ya shule na vyuo.

### Madhumuni

Kuwa na miundombinu stahiki inayokidhi mahitaji ya wote katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

### Tamko

*5.8.5 Serikali itahakikisha uwepo wa miundombinu ya kutosheleza mahitaji ya utoaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote.*

*5.8.6 Utaratibu wa uhifadhi, utunzaji na matengenezo ya miundombinu utakuwa sehemu ya utoaji wa elimu na mafunzo.*

### Ugharimiaji wa Elimu na Mafunzo

Serikali inagharimia utoaji wa elimu na mafunzo kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wa ndani na nje. Ugharimiaji huo hufanyika kwa njia ya ruzuku inayotolewa na Serikali; misaada na mikopo inayotolewa na washirika wa maendeleo; ujenzi na uendeshaji wa shule unaofanywa na jamii na sekta binafsi na mashirika yasiyo ya serikali; karo, ada na michango mingine ya hali na mali inayotolewa na wazazi na wanafunzi.

### Suala

Uwezo wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo.

### Maelezo

Moja ya majukumu ya serikali ni kutoa na kugharimia elimu na mafunzo kwa njia ya ruzuku ambayo hutokana na kodi, misaada na mikopo. Mapato ya serikali hayatoshelezi kutoa huduma hiyo kwa ukamilifu. Kwa hiyo, jamii haina budi kutambua kwamba jukumu la kutoa elimu bora ni la wananchi wote na wanawajibika kulipa kodi na kuchangia gharama ili kufanikisha utoaji wa elimu na mafunzo.

### Madhumuni

Kuimarisha uwezo wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo.

Tamko

*5.8.7 Serikali itaendelea kuiweka sekta ya elimu na mafunzo kuwa moja ya vipaumbele vikuu vya nchi.*

*5.8.8 Serikali itaimarisha utoaji na urejeshaji wa mikopo kwa wanafunzi na kupanua wigo kwa kuhusisha vyombo mbalimbali vya fedha*

*5.8.9 Sekta binafsi, jamii, wazazi na watumiaji wa elimu na mafunzo watachangia gharama za elimu na mafunzo.*

*5.8.10 Gharama halisi za elimu na mafunzo kwa kila ngazi itakuwa msingi wa kupanga ada na karo kwenye taasisi za elimu na mafunzo .*

*5.8.11 Uratibu wa Mifuko ya fedha ya kugharimia elimu na mafunzo utaimarishwa, na fedha kutumika kulingana na vipaumbele vya elimu na mafunzo.*

*5.8.12 Mamlaka za Serikali za Mitaa zitatafuta vyanzo mbadala vya kugharimia elimu na mafunzo katika maeneo yao.*

# SURA YA 6

## 6.0 MASUALA MTAMBUKO

### *6.1* Utangulizi

Masuala mtambuko katika elimu ni pamoja na jinsia, mazingira, VVU/UKIMWI, Ushauri na Unasihi, haki za binadamu

, haki za mtoto, naUtawala Bora. Kwa kuwa masuala haya ni muhimu katika maendeleo ya taifa, hayana budi kuzingatiwa katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

### *6.2* Jinsia katika Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu na Mafunzo

#### Suala

Uwiano wa jinsia katika usimamizi na uendeshaji wa elimu na mafunzo.

#### Maelezo

Jinsia inahusu wajibu wa wanaume na wanawake katika jamii. Jinsia katika elimu na mafunzo inahusu usawa katika utoaji, usimamizi na uendeshaji wa elimu na mafunzo. Ushirikishwaji wa wanawake katika ngazi mbalimbali za usimamizi na uongozi ni mdogo kutokana na fikra potofu katika jamii kuwa wanawake hawana uwezo sawa na wanaume. Kuna umuhimu wa kuweka usawa wa ushiriki katika usimamizi na uendeshaji wa elimu na mafunzo kwa ngazi zote.

#### Madhumuni

Kuwa na usawa wa kijinsia katika usimamizi na uendeshaji wa elimu na mafunzo.

#### Tamko

*6.2.1 Serikali itaweka utaratibu wa usimamizi na uongozi wa elimu na mafunzo unaozingatia sifa stahiki na usawa wa kijinsia.*

### *6.3* Elimu ya Mazingira na Afya ya Jamii

#### Suala

Utoaji wa Elimu ya mazingira na Afya ya Jamii

#### Maelezo

Elimu ya mazingira na afya ya jamii inawezesha jamii kuelewa, kuthamini na kutunza mazingira. Elimu hii huwezesha jamii kupata maarifa, stadi na mwelekeo utakaomsaidia kuwa mbunifu katika kutatua matatizo ya mazingira na kuongeza ubora wa afya ya jamii. Ongezeko la idadi ya watu na shughuli mbalimbali za huduma ya kijamii na za uchumi zisizozingatia taratibu zinazofaa zimesababisha uharibifu wa mazingira nchini. Hii ni pamoja na ukataji ovyo wa miti, uchafuzi wa hewa, uharibifu wa vyanzo vya maji, utupaji ovyo wa maji-taka, taka-ngumu na taka-sumu; na matumizi mabaya ya ardhi yaliyokithiri katika maeneo mengi. Hali hii ikiendelea itahatarisha maisha ya binadamu na viumbe vilivyopo na kuathiri maendeleo ya nchi. Elimu itolewayo shuleni na vyuoni haina budi kumjengea mwanafunzi tabia na utamaduni stahiki kuhusu utunzaji wa mazingira na afya ya jamii.

Afya ya jamii inakabiliwa na matatizo na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na mazingira hatarishi, mitindo duni ya maisha na ukosefu wa maadili yanayosababisha matatizo mbalimbali ya afya. Matatizo hayo ni pamoja na saratani, shinikizo la damu, kiharusi, kisukari, VVU/UKIMWI, kifua kikuu, malaria, matumizi mabaya ya dawa za kulevya na lishe duni. Elimu itolewayo haina budi kuzingatia umuhimu wa kumjengea mwanafunzi na jamii tabia na mwenendo stahiki.

#### Madhumuni

Kuwa na jamii yenye Maarifa, Stadi na Utamaduni wa kutunza mazingira na afya ya jamii.

#### Tamko

*6.3.1 Serikali itaendelea kutoa elimu ya mazingira na afya ya jamii.*

*6.3.2 Elimu ya mazingira na afya ya jamii itaendelea kuwa sehemu ya mitaala ya elimu na mafunzo.*

## *6.4 Ushauri na Unasihi katika Elimu na Mafunzo*

### Suala

Utoaji wa huduma ya ushauri na unasihi katika elimu na mafunzo.

### Maelezo

Huduma ya ushauri na unasihi inalenga kumwezesha mwanafunzi na jumuiya ya shule kwa ujumla kukabiliana na changamoto za maisha ili kujenga mwelekeo, tabia na kuendeleza mila, desturi na maadili mema katika jamii. Kutokana na utandawazi, kumekuwa na mwingiliano wa utamaduni na hivyo kusababisha mmomonyoko wa maadili katika jamii. Huduma za ushauri na unasihi zinahitajika kwa wafanyakazi na wanafunzi katika ngazi zote za elimu ili waweze kupata stadi za maisha za kujitambua na kufanya maamuzi sahihi katika kutekeleza wajibu wao kikamilifu.

Ingawa Serikali imeweka utaratibu wa kutoa huduma za ushauri na unasihi katika shule na vyuo, utoaji wa huduma hiyo haukidhi mahitaji.

### Madhumuni

Kuwa na huduma ya ushauri na unasihi inayokidhi mahitaji katika elimu na mafunzo.

### Tamko

*6.4.1 Serikali itaimarisha utoaji wa huduma ya ushauri na unasihi katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

*6.4.2 Ushauri na unasihi utaendelea kuwa sehemu muhimu ya*

*mitaala ya Elimu ya Ualimu.*

## *6.5* Haki za binadamu katika elimu na Mafunzo

### Suala

Haki za binadamu katika utoaji wa elimu na mafunzo

### Maelezo

Msingi wa haki za binadamu umejengwa katika Azimio la Umoja wa Mataifa lenye vifungu 30 la tarehe 10 Desemba mwaka 1948. Haki hizo ni pamoja na haki ya haki ya kuzaliwa, kuwa na utaifa, kuishi, fursa na usawa katika kupata huduma za jamii, kupata elimu, kuwa huru na salama, kutoa mawazo, kuwa na dhamiri na kuabudu.

Jitihada mbalimbali za kuzingatia haki za binadamu zimeainishwa katika mipango na mikakati ya utoaji wa elimu na mafunzo. Hata hivyo, hali ya mazingira na upatikanaji wa rasilimali baadhi ya haki za binadamu zimekuwa hazizingatiwi kikamilifu katika utoaji wa elimu na mafunzo.

### Madhumuni

Kutoa elimu kwa kuzingatia Haki za Binadamu.

### Tamko

*6.5.1* *Haki za binadamu zitatambuliwa na kuthaminiwa katika mfumo wa elimu na mafunzo*

*6.5.2* *Elimu kuhusu haki za binadamu itazingatiwa katika mitaala ya elimu na mafunzo.*

## *6.6* Haki za mtoto

### Suala

Haki na wajibu wa mtoto katika utoaji wa elimu

### Maelezo

Watoto ni kundi kubwa katika jamii ambalo halina uwezo wa kujilinda dhidi ya uonevu wa aina mbalimbali. Haki za mtoto ni stahili maalumu ambazo mtoto anazaliwa nazo na anapaswa kufurahia kwa sababu tu yeye ni binadamu. Ni haki za msingi za binadamu walio kwenye hatua za makuzi kiakili na kimaumbile. Haki hizi zinahusisha maeneo makuu matatu yaani; haki za kupatiwa mahitaji muhimu ya kimaisha kama vile chakula, mavazi, malazi, elimu na fursa nyingine; haki za kulindwa dhidi ya maradhi, uonevu, udhalilishwaji, ubaguzi, ukatili wa aina yoyote na haki ya kushirikishwa kwenye masuala mbalimbali yanayowahusu.

Uimarishaji wa utoaji wa haki ya mtoto shuleni ni muhimu katika kufikia malengo ya usawa, demokrasia na kuondoa ubaguzi na migogoro shuleni. Aidha, kufanikisha haki ya mtoto kunafanya mchakato wa kufundisha na kujifunza kuwa na uhuru mpana wa kuruhusu fikra na vipaji vya mtoto kuchanua, kuimarisha ushirikishwaji, kukuza amani, furaha na mshikamano zaidi miongoni mwa wanafunzi, wanafunzi na walimu pamoja na wanafunzi na wadau wengine wa elimu katika kufanikisha malengo ya elimu na mafunzo kwa Tanzania.

Hivyo, kuna umuhimu wa kuwa na mfumo wa elimu unaozingatia haki ya mtoto na unaoweka bayana wajibu wa jamii na watoto wenyewe katika utekelezaji wa haki hizo.

### Madhumuni

Kuwa na mfumo unaozingatia Haki na wajibu wa mtoto katika utoaji wa elimu .

### Tamko

*6.6.1 Haki za mtoto zitatambuliwa, zitalindwa na kuthaminiwa katika mfumo wa elimu na mafunzo*

*6.6.2 Serikali itahakikisha kuwa mtoto anapewa haki ya elimu, analindwa na kushirikishwa katika maamuzi ya kielimu.*

## *6.7* Utawala Bora katika Mfumo wa Elimu na Mafunzo

### Suala

Maadili katika elimu na mafunzo.

Maelezo

Utawala bora unajumuisha uongozi, usimamizi na uendeshaji unaozingatia utawala wa sheria, uadilifu, uwajibikaji, uwazi, ushirikishwaji na usawa ili kufikia malengo. Utawala bora unapatikana kwa kuzingatia maadili ya kazi na utendaji katika uongozi na utawala. Utawala bora ni muhimu katika kuwawezesha watendaji na wanafunzi kutumia vizuri rasilimali zilizopo ili kufikia malengo ya elimu na mafunzo. Mmomonyoko wa maadili na kutowajibika ipasavyo kwa watendaji na wanafunzi husababisha kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Madhumuni

Kuwa na utawala bora katika elimu na mafunzo

Tamko

*6.7.1 Serikali itasimamia utekelezaji wa sheria, kanuni na taratibu zitakazowezesha utawala bora katika elimu na mafunzo.*

*6.7.2 Maadili ya utumishi yataimarishwa katika utoaji wa elimu na mafunzo*

SURA YA 7

# 7.0 MUUNDO WA KITAASISI

## *7.1* Utangulizi

Sera ya Elimu na Mafunzo itatekelezwa katika ngazi za elimu ya msingi, sekondari, ualimu, ufundi na elimu ya juu. Ili kufikia azma hiyo, Wizara yenye dhamana ya Elimu na Mafunzo itashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa (OWM – TAMISEMI), wizara nyingine, mashirika na taasisi za Serikali na zisizo za Serikali, washirika wa maendeleo wa ndani na nje, jamii na wadau wengine wa elimu na mafunzo. Aidha, Sera ya Elimu na Mafunzo itatekelezwa kiutawala na kiutendaji katika ngazi za; Taifa, Mkoa, Mamlaka za Halmashauri, Kata, Shule na Vyuo.

## *7.2* Ngazi ya Taifa

Katika kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo, Wizara yenye dhamana ya elimu na mafunzo itakuwa na muundo wa kitaasisi utakaojumuisha elimu ya msingi, sekondari, elimu ya watu wazima, ualimu, ufundi na elimu ya juu. Aidha, wizara yenye dhamana ya elimu itashirikiana na wizara yenye dhamana ya tawala za mikoa na serikali za mitaa pamoja na wizara na taasisi nyingine katika utekelezaji wa sera.

## *7.3* Ngazi ya Mkoa

Jukumu la mkoa ni kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria, kanuni na miongozo ya elimu na mafunzo katika ngazi ya halmashauri. Mkoa utawajibika katika kuratibu utekelezaji wa mipango ya halmashauri, kutathmini na kutoa taarifa ya utekelezaji wa sera kwa ngazi ya taifa. Katika kutekeleza majukumu yake ngazi ya mkoa itahitaji kuwa na timu ya uongozi wa elimu na mafunzo yenye nyenzo muhimu na wataalamu wa elimu katika kutekeleza majukumu yake.

## *7.4* Halmashauri za Wilaya, Mji, Manispaa na Jiji

Ngazi ya Halmashauri itahusika katika usimamizi na uendeshaji wa elimu na mafunzo katika eneo lake. Ngazi hii itasimamia moja kwa moja uendeshaji wa shule

za msingi na sekondari zilizoko katika halmashauri hiyo na utoaji wa elimu ya watu wazima. Halmashauri itasimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo kwa kufuata sheria, kanuni na miongozo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Halmashauri itawajibika katika kupanga, kuratibu, kutekeleza, kutathmini na kutoa taarifa ya utekelezaji wa sera kwa ngazi za mkoa na Taifa. Hivyo, Halmashauri inatakiwa kuwa na timu ya uongozi wa elimu na mafunzo yenye uwezo na nyenzo za kutekeleza majukumu hayo.

### *7.5* Ngazi ya Kata

Ngazi ya Kata itahusika na uratibu wa utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo katika ngazi hiyo. Kata itawajibika katika kuratibu utekelezaji wa mipango ya shule za msingi, sekondari na elimu ya watu wazima na kutoa taarifa ya utekelezaji wa sera kwa ngazi ya Halmashauri. Utekelezaji wa majukumu hayo yatahitaji mtaalamu wa elimu mwenye uwezo stahiki.

### *7.6* Ngazi ya Shule na Chuo

Ngazi ya shule na chuo itahusika na usimamizi na uendeshaji wa siku hadi siku wa shule na chuo. Mkuu wa shule ya msingi na wa shule ya sekondari atasimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo katika shule na atawajibika kupanga, kusimamia utekelezaji kwa kushirikiana na mamlaka ya kijiji/ mtaa na kutoa taarifa za utekelezaji kwa Kata na Halmashauri . Mkuu wa chuo cha ualimu, chuo cha elimu ya ufundi, chuo cha mafunzo ya ufundi stadi na chuo kikuu atapanga, atasimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo katika chuo na kutoa taarifa za utekelezaji kwa mamlaka zilizo juu yake.

SURA YA 8

# 8.0 MUUNDO WA KISHERIA

## *8.1* Sheria ya Kusimamia Elimu na Mafunzo

Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo utakuwa na muundo wa kisheria utakaowawezesha wahusika kutekeleza majukumu yao. Sheria mbalimbali zinazohusu elimu na mafunzo nchini zitapitiwa upya na kufanyiwa marekebisho au kufutwa. Mapitio ya sheria hizo yatazingatia muundo wa kitaasisi ulioainishwa katika sera hii, vyombo vitakavyoanzishwa na makubaliano yaliyopo kwenye mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa juu ya haki ya kupata elimu.

Sekta za Serikali na zisizo za Serikali zinazojishughulisha na utoaji wa elimu na mafunzo zitatakiwa kufuata sheria, kanuni, taratibu na miongozo itakayotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo.

## *8.2* Vyombo vya Kisheria vya Kusimamia Elimu na Mafunzo

Kutakuwepo na vyombo vya kisheria katika ngazi zote ili kusimamia utekelezaji wa elimu na mafunzo katika maeneo hayo kwa mujibu wa sheria. Vyombo hivyo vitasimamia: taaluma, utaalamu na maadili ya ualimu; utoaji wa huduma za maktaba; ulinganifu wa sifa za kitaaluma; rasilimali fedha kwa ajili ya ugharimiaji wa elimu na mafunzo na ushauri wa elimu na mafunzo.

## *8.3* Sheria ya Kusimamia Shule na Vyuo vya Elimu na Mafunzo

Shule za msingi, sekondari, vyuo vya elimu ya ufundi, vyuo vya ufundi stadi, vyuo vya ualimu, na vyuo vikuu vitatambuliwa kisheria na kuundiwa vyombo vya usimamizi. Shule za msingi zitasimamiwa na kamati za shule, na shule za sekondari, vyuo vya ualimu, vyuo vya ufundi na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi vitasimamiwa na bodi. Vyuo vikuu vitasimamiwa na vyombo vitakavyoundwa kwa mujibu wa sheria.

Kutakuwa na mamlaka za rufaa katika ngazi za halmashauri na mkoa kwa ajili ya

mashauri ya shule za msingi na sekondari. Mamlaka za rufaa kwa ajili ya vyuo vya elimu ya ufundi, vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi na vyuo vikuu zitaundwa kwa mujibu wa sheria.

# SURA YA 9

## 9.0 HITIMISHO

Sera hii ya Elimu na Mafunzo imeandaliwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali. Madhumuni ya sera hii ni kutoa mwongozo wa jumla wa uendeshaji wa elimu na mafunzo kwa mtazamo wa kiulimwengu na kiteknolojia katika maeneo ya mfumo na muundo, fursa na usawa, mitaala, upimaji, menejimenti, uongozi, masuala mtambuko na muundo wa kitaasisi.

Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo utahitaji maandalizi ya mikakati na mipango mbalimbali kwa kuzingatia matakwa ya Sera. Watekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo katika ngazi zote watatumia miongozo ya utekelezaji wa sera. Utekelezaji fanisi wa Sera ya Elimu na Mafunzo utahitaji mfumo thabiti wa ufuatiliaji na tathmini utakaoshirikisha wadau katika kila ngazi kwa kuzingatia viashiria stahiki vya Elimu na Mafunzo. Aidha, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ni nyenzo muhimu itakayopima nchi imetoka wapi, iko wapi, na inakwenda wapi katika utoaji wa elimu na mafunzo.